
2025
Januari - Machi

Gombo la. 101, Na. 1

MASOMO YA BIBLIA YA SHULE SABATO

WATU WAZIMA



SEHEMU YA KWANZA

# Injili Kulingana na Yohana

Mwanafunzi huyo mpendwa anamtambulisha Yesu Kristo, Mwana wa milele wa Mungu na dawa ya kiungu ya dhambi ya ulimwengu mzima.

# Yaliyomo

SHULE YA SABATO


1. Injili kulingana na Yohana....................................5
2. Mwanakondoo wa Mungu....................................10
3. Harusi ya kana....................................15
4. Yesu Hekaluni....................................20
5. Yesu na Nikodemo....................................26
6. Mguso wa Roho Mtakatifu....................................31
7. Yesu na Yohana Mbatizaji....................................36
8. Yesu na Mwanamke Msamaria....................................41
9. Kuzaliwa kwa Mmisionari....................................47
10. Yesu na mwana wa Diwani....................................52
11. Yesu na mwenye kupooza wa Bethzatha....................57
12. Mamlaka ya Mwana....................................62
13. Yesu kuwalisha makutano....................................67


**Masomo ya Biblia ya shule ya sabato** ni utaratibu wa mafundisho ya kila siku, msingi wake pekee ni juu ya Biblia na Roho ya Unabii pasipo maelezo ya nyongeza. Nukuu itolewe kwa ufupi kadri iwezekanavyo, ili kuelekeza ufahamu. [ ] mabano huwekwa baadhi ya sehemu ili kusaidia kuelewa jambo kwa usahihi. Jifunze zaidi katika chanzo kilichopendekezwa.


Masomo ya shule ya sabato (USPS 005 - 118), Gombo la 101, Toleo Na. 1, Januari - Machi 2025 imechapishwa na Baraza kuu Ulimwenguni (GC) - Seventh Day Adventist Reform Movement, Idara ya shule ya sabato.


Nakala zote©2025, zinachapishwa na kusambazwa na Reformation Herald Publishing Association, 5240 Hollins Road, Roanoke, Virginia 24019 - 5048, U.S.A Virginia 24022-9993. nchini Marekani.



Imetafsiriwa na: **SDA Reform Movement, Tanzania Mission,** Idara ya shule sabato, S.L.P 1342, DODOMA TANZANIA

# Utangulizi

Mwaka huu, tutakuwa tukijifunza mara nne kwa robo juu ya Injili Kulingana na Yohana. Kwa unyenyekevu, mwandishi wa injili ya nne hajitambulishi mwenyewe, wala hajielekezi kuwa wale wanafunzi wawili wakamsikia akinena,wakamfuata Yesu(Yohana 1:37). Badala yake, anarejelea "mwanafunzi mwingine," "mwanafunzi huyo," "mwanafunzi . . . ambaye alimpenda," "mwanafunzi ambaye Yesu alimpenda," na "mwanafunzi anayeshuhudia mambo haya" ( Yohana 18:15; 19:26; 21:20, 23, 24 ). Ukweli kwamba wanafunzi wengine mashuhuri wanatajwa kwa majina huku jina la Yohana likiachwa, inaonekana kuashiria kwamba lazima alikuwa mwandishi wa injili hiyo.

Kulingana na Roho ya Unabii, mwandishi wa injili ya nne alikuwa Yohana, "mwanafunzi ambaye Yesu alimpenda." Alikuwa mmoja wa wanafunzi watatu walioshuhudia utukufu wa Kristo juu ya mlima wa kugeuka sura na uchungu Wake katika bustani mara tu kabla ya kukamatwa Kwake. Maisha yake ni kielelezo chenye kujitokeza kinachoonyesha jinsi nguvu za Mungu zinavyoweza kumgeuza kikamili "mwana wa ngurumo" kuwa mtu mwenye tabia ya upendo na ufahamu wa kina wa kiroho.

"Yohana alishikamana na Kristo kama vile mzabibu unavyoshikamana na nguzo kuu. Kwa ajili ya Bwana wake alistahimili hatari za jumba la hukumu na kukaa karibu na msalaba, na kwa habari ya kwamba Kristo amefufuka, aliharakisha kwenda kaburini, katika bidii yake kumvua hata Petro mwenye hasira.

"Upendo wa siri na ujitoaji usio na ubinafsi unaodhihirishwa katika maisha na tabia ya Yohana hutoa masomo ya thamani yasiyoelezeka kwa kanisa la Kikristo. Yohana hakuwa na kawaida ya kupendeza ya tabia ambayo uzoefu wake wa baadaye ulifunua. Kwa asili alikuwa na kasoro kubwa. Hakuwa tu mwenye kiburi, mwenye kujidai, na mwenye shauku ya kupata heshima, bali alikuwa na hasira, na mwenye kinyongo chini ya jeraha. Yeye na ndugu yake waliitwa 'wana wa ngurumo.' Hasira mbaya, tamaa ya kulipiza kisasi, roho ya kuchambua, yote yalikuwa ndani ya mwanafunzi huyo mpendwa. Lakini chini ya haya yote Mwalimu wa kimungu alitambua moyo wa bidii, mnyoofu, na upendo. Yesu alikemea ubinafsi huo, akakatisha tamaa yake, akajaribu imani yake. Lakini Alimfunulia yale ambayo nafsi yake ilitamani—uzuri wa utakatifu, nguvu inayogeuza upendo." — *The Acts of the Apostles,* pp. 539, 540.

Mamlaka zote za kale zinasema kwamba injili ya Yohana iliandikwa huko Efeso karibu A.D. 90 au mapema zaidi. Mwanafunzi huyo alikuwa ametiwa ndani ya sufuria ya mafuta yaliyokuwa yakichemka na akaepuka kifo kwa njia ya kimuujiza, na baadaye alifukuzwa kwenye kisiwa cha Patmo (Ufunuo 1:9). Hapo aliandika Ufunuo. Kupaa kwa Nerva kwenye kiti cha enzi (AD 96) kulifanya iwezekane kwake kurudi Efeso, ambako inaaminika kwamba aliendelea kuishi hadi kifo chake wakati wa utawala wa Trajan (a.d. 98–117).

Roho wa Kristo na aongoze masomo yetu robo hii, na aguse mioyo yetu kwa kuitikia upendo Wake!

*Idara ya Shule ya Sabato GC*

# Sadaka ya Sabato ya Kwanza

Sabato, Tarehe 4 Januari 2025

### Kituo cha Madhumuni mengi cha Afya na Elimu nchini Paraguay




Jamhuri ya Paraguay ni nchi isiyo na bandari katika Amerika Kusini, ambapo inapakana na Argentina, Bolivia, na Brazili. Idadi ya watu ni takriban wakaaji milioni 6.1, 96.1% kati yao wanadai Wakristo (88.3% wakatoliki na 7.8% imani zingine za Kikristo); 2.6% wanadai hawana dini, na waliosalia ni wa dini zingine au hawakutaja. Uchumi wa kitaifa unategemea kilimo hasa soya na katika miaka 50 iliyopita, Paragwai pia imekuza tasnia kubwa ya umeme wa maji.

Washiriki wa kwanza wa SDA Reform Movement waliwasili hapa kutoka Hungaria katika miaka ya 1940 na kazi ikapanuka zaidi katika miaka ya 1950 kupitia huduma ya ukolpota na baadaye katika miaka ya 1970. Kupitia kazi ya umishonari ya matibabu. Kwa sasa tuna kundi la ajabu la washiriki waaminifu katika miji mikuu.

Kwa miaka mingi tulikuwa na kituo cha afya cha asili kinachofanya kazi katika mji mkuu wa Asunción, kikituwezesha kushiriki injili na nafsi nyingi na kufundisha mtindo wa maisha wa masalia ya watu wa Mungu. Kwa msaada wa Mungu na timu yetu ya wataalamu wa taaluma mbalimbali, tunatumai kufufua zahanati hiyo—lakini sasa ili ifanye kazi kama uhamasishaji katika jiji, pamoja na upanuzi wa vijijini

kutimiza agizo la kimungu: "'Ondokeni nje ya majiji. Weka vituo vyako vya usafi, shule zako, na ofisi zako mbali na maeneo yenye idadi ya watu.' "—*Selected Messages,* bk. 2, uk. 357

Tukiwa na ono hilo akilini, tulipata ardhi katika eneo la vijijini lenye kuvutia sana katika idara ya Paraguarí, karibu kilomita 66 (maili 41) kutoka mji mkuu. Tayari tuna kanisa na nyumba ya watendakazi katika eneo, lakini huu ni mwanzo tu. Lengo ni kuanzisha kituo chenye kazi nyingi chenye kituo cha afya cha msingi, shule ya kanisa, kanisa, na kituo cha maendeleo ya biashara ya chakula cha afya inayojitegemea.

Tunaomba ukarimu wa ndugu zetu duniani kote watusaidie kutimiza lengo hili. Ushirikiano wako utafanya iwezekane kutoa msukumo mpya kwa awamu ya mwisho muhimu ili kukamilisha mradi. Tunapumzika katika uwezo na neema ya ajabu ya mungu na tuna hakika kwamba Bwana atabariki juhudi za jumuiya yetu duniani kote kuwezesha na kupanua uinjilist katika sehemu hii ya shamba la mizabibu.

*Ndugu zenu kutoka Field ya Paraguayan*

Sabato, Januari 4, 2025

**Somo la 1**

# Injili Kulingana na Yohana

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli " ( Yohana 1:14).

**Inapendekezwa kusoma:** *Patriarchs and Prophets,* pp. 44–51, 111–116.

"Tangu milele Kristo aliunganishwa na Baba, na alipojitwalia asili ya kibinadamu, bado alikuwa mmoja na Mungu." — *Selected Messages*, bk. 1, uk. 228.

## 1. YESU, MMOJA PAMOJA NA BABA — 12/29 (Jpil)

a. a. Neno la Mungu linasema nini kuhusu Yesu kabla ya kufanyika mwili? Yohana 1:1,2.

---

---

"Tangu milele na milele Bwana Yesu Kristo alikuwa katika umoja na Baba; alikuwa "sura yake Mungu," sura ya ukuu na uweza wake, „mng'ao wa utukufu wake." Alikuja katika ulimwengu wetu ili kudhihirisha utukufu huo. Alikuja katika dunia hii ya giza kuifunua nuru ya upendo wa Mungu, - alikuja kuwa "Mungu pamoja nasi." — *The Desire of Ages,* p. 19.

"Kristo aliye Neno, mwana pekee wa Mungu, alikuwa mmoja na Baba wa milele — katika asili, katika tabia, katika kusudi—kiumbe pekee ambacho kingeweza kuingia katika mashauri na makusudi yote ya Mungu."— *Patriarchs and Manabii*, uk. 34.

b. Yesu alizingatiwaje na Baba na malaika? Zaburi 45:6; Isaya 9:6; Waebrania 1:3, 6–8.

---

---

"Malaika ni wahudumu wa mungu, waking'aa kwa nuru inayotiririka daima kutoka kwa uwepo wake na wakienda kasi kwa mrengo wa haraka ili kutekeleza mapenzi yake. Lakini Mwana, mpakwa mafuta wa Mungu, 'mfano wazi wa nafsi yake,' 'mng'ao wa utukufu wake', akivishikilia vitu vyote kwa neno la uweza wake,' ana ukuu juu ya vyote." – Ibid.

## 2. MCHAKATO WA UUMBAJI

12/30 (jtatu)

**a. Ni nani aliyeumba vitu vyote? Yohana 1:3,10; Wakolosai 1:15–17; Waebrania 1:2.**

“Ni Kristo aliyetandaza mbingu hizi, na aliweka msingi wa dunia. Ni mkono wake ulioning’iza malimwengu angani, na kuyapamba maua ya kondeni. „Milima aliiweka imara kwa nguvu zake.” Zaburi 65:6; 95:5. Ni Yeye aliyeijaza dunia kwa uzuri, na anga kwa wimbo. Na akaandika ujumbe wa pendo la Baba kwenye vitu vyote vilivyo duniani, hewani, na angani. Aliandika ujumbe wa upendo wa baba” —Ibid. — *The Desire of Ages*, p. 20.

**b. Elezea jinsi gani ulimwengu na vilivyomo uliumbwa. Zaburi 33:6, 9; 104:1–6.**

“Mungu alinena, na maneno Yake yakaumba kazi Zake katika ulimwengu wa asili. Uumbaji wa Mungu ni hifadhi tu ya njia iliyotayarishwa kwa ajili Yake ili aitumie mara moja kufanya mapenzi Yake.” — *The SDA Bible Commentary [E. G. White Comments],* juz. 1, uk. 1081.

“Dunia ilipotoka mkononi mwa Muumba wake, ilikuwa nzuri sana. Uso wake ulikuwa na milima mbalimbali, vilima, na tambarare, ukiwa na mito mikuu na maziwa mazuri; lakini vilima na milima haikuwa na mipasuko, iliyojaa miinuko ya kutisha na mashimo ya kutisha, kama ilivyo sasa; kingo zenye ncha kali za miamba ya dunia zilizikwa chini ya udongo wenye rutuba, ambao kila mahali ulitokeza ukuaji wa mimea mizuri ya kijani. Hakukuwa na mabwawa mabaya au majangwa tupu. Vichaka vya kupendeza na maua maridadi yakikutana kila upande. Miinuko ilipambwa kwa miti mikubwa zaidi kuliko hata iliyopo sasa. Hewa, isiyochafuliwa na hewa chafu ya magonjwa, ilikuwa safi na yenye afya. Mazingira yote yalizidi kwa uzuri uwanja uliopambwa wa ikulu ya fahari zaidi. Jeshi la malaika lilitazama manzari hiyo kwa furaha, na kushangilia kazi za ajabu za Mungu.” — *Patriarchs and Prophets,* p. 44.

“Biblia haitambui enzi nyingi ambazo katika hizo dunia ilibadilishwa polepole kutoka kwa machafuko. Katika kila siku iliyofuatana ya uumbaji, kumbukumbu takatifu inatangaza kwamba ilitia ndani jioni na asubuhi, kama siku nyingine zote ambazo zimefuata. Mwishoni mwa kila siku hutolewa matokeo ya kazi ya Muumba.” — *Ibid.,* p. 112.

## 3. NURU YA ULIMWENGU — 1/31 (jnne)

**a. Ni nani Mwanzilishi wa uhai na nuru yote — na hii inatufaidije sisi? Yohana 1:4–9; Matendo 17:28.**

---

---

"Ni [Kristo] ambaye alikuwa amesema kupitia kila mtu kwamba katika enzi zote alikuwa ametangaza neno la Mungu kwa wanadamu. Kutoka Kwake utukufu wote uliodhihirika katika nafsi kuu na adhimu za dunia ulikuwa ni tafakari." — *Education,* p. 73I

"Kristo ndiye 'Nuru, amtiaye nuru kila mtu ajaye ulimwenguni.' Yohana 1:9. Kama vile kupitia Kristo kila mwanadamu ana uzima, vivyo hivyo kupitia Kwake kila nafsi inapokea baadhi ya miale ya nuru ya kimungu."— *Ibid.,* p. 29.

"Nguvu za Mungu bado zinatumika katika kutegemeza vitu vya uumbaji Wake. Sio kwa sababu utaratibu unaowekwa mara moja unaendelea kufanya kazi kwa nishati yake ya asili ambayo mapigo hupiga, na pumzi hufuata pumzi. Kila pumzi, kila mdundo wa moyo, ni ushahidi wa utunzaji wa Yeye ambaye ndani yake tunaishi na kusonga na kuwa na uhai wetu. Kuanzia kwa mdudu mdogo hadi kwa mwanadamu, kila kiumbe hai kinategemea riziki yake kila siku. . . .

"Nguvu kuu inayofanya kazi kupitia maumbile yote na kutegemeza vitu vyote si, kama baadhi ya wanasayansi wanavyodai, kanuni iliyoenea tu, nishati inayofanya kazi. Mungu ni roho; lakini Yeye ni kiumbe binafsi, kwa maana mwanadamu aliumbwa kwa mfano Wake. Kama kiumbe binafsi, Mungu amejidhihirisha katika Mwanawe." — *Ibid.,* p. 131.

**b. Yesu anasema nini kuhusu Mwenyewe? Yohana 9:5; 8:12; 3:19; 12:46.**

---

---

"Katika maneno, "Mimi ndimi nuru ya ulimwengu," Yesu alijitangaza kama Masihi. Yule kikongwe Simeoni, katika hekalu hili hili ambamo sasa Yesu alikuwa anafundisha, alikuwa amepata kumtaja Yeye kama "nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa, na kuwa utukufu wa watu wako Israeli." Luka 2:32. Katika maneno haya alikuwa anamhusianisha na unabii uliokuwa unafahamika kwa Israeli wote. Kupitia nabii Isaya, Roho Mtakatifu alikuwa ametangaza kwamba, "Ni neno dogo sana wewe kuwa mtumishi wangu ili kuziinua kabila za Yakobo, na kuwarejeza watu wa Israeli waliohifadhiwa; zaidi ya hayo nitakutoa uwe nuru ya mataifa, upate kuwa wokovu wangu hata miisho ya dunia." Isaya 49:6. Unabii huu ulieleweka kwa ujumla kwamba ulimhusu Masihi, na Yesu aliposema, "Mimi ndimi nuru ya ulimwengu," watu hawakushindwa kugundua dai lake la kuwa Yeye Aliyeahidiwa." — *The Desire of Ages*, p. 465.

## 4. MUNGU PAMOJA NASI — 2/1 (Jtano)

a. Isaya alitabiri nini kuhusu jina la Kristo? Isaya 7:14. Unabii huu ulitimizwa lini? Mathayo 1:22, 23.

"Kwa kuwa Yesu alikuja kukaa nasi, tunajua kwamba Mungu anafahamu majaribu yetu, na anatuonea huruma katika shida zetu. Kila mwana na binti wa Adamu ajue kwamba Muumba wetu ni rafiki wa wenye dhambi. Maana katika kila fundisho la neema, kila ahadi ya raha, kila tendo la upendo, kila mvuto wa kimbingu ulioonyeshwa katika maisha ya Mwokozi alipokuwa duniani, tunamwona "Mungu pamoja nasi." — *The Desire of Ages,* p. 24.

b. Yesu alifanya nini ili kutufikia katika hali yetu ya kuanguka? Yohana 1:14; Wafilipi 2:5–8; Waebrania 2:14–18.

"Ili tupate kufahamu tabia na uzima Wake wa kiungu, Kristo alichukua asili yetu na kukaa kati yetu. Uungu ulifunuliwa katika ubinadamu; utukufu usioonekana katika umbo la kibinadamu linaloonekana. Watu wangeweza kujifunza mambo yasiyojulikana kupitia yanayojulikana; mambo ya mbinguni yalifunuliwa kwa njia ya dunia; Mungu alidhihirishwa katika sura ya wanadamu."— *Christ's Object Lessons*, p. 17.

"Mwana wa Mungu alishambuliwa kwa kila hatua na nguvu za giza. Baada ya ubatizo wake alifukuzwa na Roho nyikani, akapata majaribu kwa muda wa siku arobaini. Kama Yeye hakuwa mshiriki wetu wa asili, Hangeweza kujaribiwa kama mwanadamu. Kama isingewezekana kwake kukubali majaribu, hangeweza kuwa msaidizi wetu. Ilikuwa ni ukweli mzito kwamba Kristo alikuja kupigana vita kama mwanadamu, kwa niaba ya mwanadamu. Majaribu na ushindi wake hutuambia kwamba ubinadamu lazima uige Mfano; mwanadamu lazima awe mshiriki wa asili ya kimungu."— *The SDA Bible Commentary [E. G. White Comments],* juz. 5, uk. 1082.

"Kuweka utukufu Wake ukiwa umefunikwa kama mtoto wa jamii iliyoanguka, hii ilikuwa nidhamu kali zaidi ambayo Mkuu wa uzima angeweza kujitiisha kwayo. Hivyo akapima nguvu zake kwa Shetani. Yeye ambaye alikuwa amefukuzwa kutoka mbinguni alipigana sana kwa ajili ya kumshinda Yule ambaye katika mahakama za juu alikuwa amemwonea wivu. Ilikuwa vita gani hivi! Hakuna lugha ya kutosha kuielezea. Lakini katika siku za usoni itaeleweka kwa wale ambao wameshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo na neno la ushuhuda wao." — *Ibid.,* uk. 1081, 1082.

## 5. KUSUDI LA KUFANYIKA MWILI — 2/2 (Alham)

a. Yesu alikuja kufanya nini kwa ajili ya wanadamu? Yohana 3:16, 17; 1:12; Luka 19:10.

---

---

"Kristo alitendewa vile tulivyostahili kutendewa sisi, ili ya kwamba tutendewe vile anavyostahili kutendewa Yeye. Alihukumiwa kwa dhambi zetu, ambazo hakuwa na sehemu katika hizo, ili tupate kuhesabiwa haki kwa haki yake, ambayo hatukuwa na sehemu ndani yake. Alikufa kifo kilichokuwa chetu, kusudi tupokee uzima uliokuwa wake. "Kwa kupigwa kwake tumepona." — *The Desire of Ages,* p. 25.

b. Je, tunarejeshwaje na dhabihu ya Kristo? Wagalatia 4:5–7; Waebrania 2:10.

---

---

"Kristo alilipa gharama kamili na timilifu, gharama inayotosha kumuokoa kila mtoto wa kike na wa kiume wa Adamu ambaye ataonesha ungamo kwa Mungu kwa kukiuka sheria Yake na kudhihirisha imani katika Bwana wetu Yesu Kristo. Kristo ni nahodha wa wokovu wetu, na kwa mateso na kafara Yake Ametupatia kielelezo kwa wafuasi wake wote kwamba kukesha na kuomba, na juhudi katika kustahimili mateso, ilikuwa ni jambo la muhimu kwao endapo wanahitaji kuakisi upendo ambao upo Kifuani Mwake kwa jamii iliyoasi." — *Testimonies for the Church,* vol. 2, p. 664.

"Mungu anawapenda watoto wake watiifu. Ana ufalme uliotayarishwa, si kwa ajili ya raia wasio waaminifu, bali kwa ajili ya watoto Wake ambao amewajaribu na kuwajaribu katika ulimwengu ulioharibiwa na kupotoshwa na dhambi. Tukiwa watoto watiifu, tuna pendeleo la kuwa na uhusiano pamoja na Mungu. 'Ikiwa ni watoto,' Asema, 'basi warithi' urithi usioweza kufa. Kristo na watu wake ni umoja. — *The SDA Bible Commentary [E. G. White Comments],* vol. 6, p. 1077.

## 6. MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI — 2/3 (ijumaa)

1. Yesu amekuwa na asili gani tangu milele?
2. Ni nani aliyezitanda mbingu na kuweka misingi ya dunia?
3. Nuru yote ya kweli hutoka kwa nani?
4. Yesu anaitwaje katika Isaya 7:14?
5. Yesu alikua nini alipochukua asili yetu ya kibinadamu?

Sabato, Januari 11, 2025

**Somo la 2**

# Mwanakondoo wa Mungu

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Alionewa, lakini alinyenyekea, wala hakufunua kinywa chake; kama mwana-kondoo apelekwaye machinjioni, na kama vile kondoo anyamazavyo mbele yao watakao manyoya yake;Naam, hakufunua kinywa chake." (Isaya 53:7).

**Inapendekezwa kusoma:** *The Desire of Ages,* pp. 132–143.

"Hebu mwenye dhambi anayetubu akaze macho yake kwa 'Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." — *The Faith I Live By,* p. 107.

## 1. USHUHUDA WA YOHANA MBATIZAJI — 1/5 (Jpil)

a. Yohana Mbatizaji alitangaza nini kuhusu Yesu? Yohana 1:15–18.

b. Je Yohana alijitambulishaje kwa viongozi wa kidini? Yohana 1:19–23. Ni unabii gani aliotimiza—na je, tutahusianaje nao? Isaya 40:3–5.

"Katika kila hatua ya historia ya dunia hii Mungu amekuwa na mawakala Wake ili kuendeleza kazi Yake, ambayo lazima ifanywe kwa njia Yake aliyoiweka. Yohana Mbatizaji alikuwa na kazi maalum, ambayo alizaliwa kwa ajili yake na ambayo aliteuliwa — kazi ya kuandaa njia ya Bwana....

"[Huduma yake ya jangwani] ilikuwa utimizo wa kushangaza zaidi, halisi wa unabii." — *The Southern Watchman*, March 21, 1905.

"Bwana alimpa [Yohana Mbatizaji] ujumbe wake. Je, aliienda kwa makuhani na watawala na kuwauliza ikiwa angeweza kutangaza ujumbe huo?— La, Mungu alimweka mbali nao ili asipate kuongozwa na roho na mafundisho yao. Alikuwa ni sauti ya mtu aliaye nyikani, [Isaya 40:3–5 imenukuliwa]. Huu ndio ujumbe wenyewe unaopaswa kutolewa kwa watu wetu; tuko karibu na mwisho wa nyakati, na ujumbe ni, Safisheni njia kuu ya Mfalme; kusanya mawe; inueni kigezo kwa watu. Watu lazima waamshwe. Sio wakati sasa wa kulia amani na usalama." — *Selected Messages,* bk. 1, p. 410.

## 2. UTUME WA DHABIHU — 1/6 (Jtat)

**a. Yesu alipokuja kwa Yohana ili abatizwe, Yohana alimtambulishaje na kushuhudia utume wake kwa makutano? Yohana 1:29, 34. Hilo lilitimiza unabii gani? Isaya 53:4–7.**

---

---

"Kristo alikuwa Mkombozi wa mwanadamu katika mwanzo wa ulimwengu kama alivyo leo. Kabla ya kuuvisha uungu Wake na ubinadamu na kuja katika ulimwengu wetu, ujumbe wa injili ulitolewa na Adamu, Sethi, Henoko, Methusela, na Nuhu. Ibrahimu katika Kanaani na Lutu katika Sodoma walibeba ujumbe, na kutoka kizazi hadi kizazi wajumbe waaminifu walitangaza Yule Ajaye. Taratibu za uchumi wa Kiyahudi zilianzishwa na Kristo Mwenyewe. Alikuwa msingi wa mfumo wao wa matoleo ya dhabihu, mfano mkuu wa huduma zao zote za kidini. Damu iliyomwagwa wakati dhabihu zilitolewa iliashiria dhabihu ya Mwana-Kondoo wa Mungu. Sadaka zote za kawaida zilitimizwa ndani Yake." — *Christ's Object Lessons*, p. 126.

**b. Je, Yohana alimtambulishaje Yesu kwa wanafunzi wake? Yohana 1:35, 36. Maneno yake yalikuwa na matokeo gani kwao—na ni nini kilichofuata maishani mwake? Yohana 1:37.**

---

---

"Siku iliyofuata,[baada ya ubatizo wa kristo] wakati wale wanafunzi wawili walipokuwa wamesimama karibu, Yohana alimwona Yesu tena akiwa miongoni mwa watu. Kwa mara nyingine sura ya nabii huyu iliwaka kwa utukufu wa Yeye asiyeonekana, na akapaza sauti akisema, "Tazama Mwana-kondoo wa Mungu!" Maneno yale yalishtua mioyo ya wanafunzi wale. Hawakuyaelewa kwa ukamilifu. Nini maana ya jina hili ambalo Yohana amempa, - „mwana-kondoo wa Mungu"? Yohana mwenyewe hakuwa amelifafanua. Walienda kumtafuta Yesu." — *The Desire of Ages,* p. 138.

"Yohana aliwafahamaisha wanafunzi wake kwamba Yesu ndiye masihi aliyeahidiwa, na mwokozi wa ulimwengu. Na kadri kazi yake ilivyokuwa ikimalizika, aliwafundisha wanafunzi wake kumgeukia Yesu, na kumfuata yeye kama mwalimu Mkuu. Maisha ya Yohana yalikuwa ya huzuni na ya kujikana nafsi. Alitangaza ujio wa Yes umara ya kwanza, lakini hakuruhusiwa kuona miujiza yake, nakufurahia nguvu zilizodhihirishwa naye. Yohana alitambua kwamba ni lazima afe wakati ambapo Yesu angejiimarisha kama Mwalimu. Sauti yake ilisikika mara chache sana isipokuwa alipokuwa jangwani. Maisha yake yalikuwa ya upweke. Hakuambatana na familia ya baba yake, kufurahia jamii yao, lakini aliwaacha ili akamilishe utume wake. " — *Early Writings,* p. 154.

## 3. WANAFUNZI WA KWANZA WA YESU 1/7 (Jnne)

**a. Ni nani waliokuwa baadhi ya wanafunzi wa kwanza wa Yesu? Mathayo 4:18,21. Walionyeshaje kupendezwa na Kristo na kwa muda gani kwa mara ya kwanza wanakutana nae? Yohana 1:38, 39.**

---

---

---

"Mmoja wa wale wawili alikuwa ni Andrea, nduguye Simoni; mwingine alikuwa Yohana mwinjilisti. Hawa ndio waliokuwa wanafunzi wa kwanza wa Yesu. Wakiwa wanasukumwa na msukumo usiopingika, walimfuata Yesu, - wakitafuta kuongea naye, lakini wakiwa kimya katika mshangao, wakiwa wamemezwa katika mawazo kwamba, "Je, huyu ni Masihi?"

"Yesu alijua kwamba wale wanafunzi walikuwa wanamfuata Yeye. Walikuwa matunda ya kwanza ya kazi yake, na kulikuwa na furaha katika moyo wa mwalimu huyu atokaye mbinguni kwa kadiri roho hizi zilivyoitikia neema yake. Hata hivyo alipogeuka, aliwauliza tu hivi, "Mnatafuta nini?" Alikuwa radhi kuwaachia uhuru wa kurudi walikotoka au waseme hitaji lao. . . . .

"Ikiwa Yohana na Andrea wangekuwa na roho ile isiyoamini ya makuhani na wakuu, wasingepatikana na kuwa wanafunzi miguuni pa Yesu. Wangemjia kama wakosoaji, ili kuhukumu maneno yake. Hivyo ndivyo wengi wanavyofungia mlango fursa za thamani kubwa sana. Lakini hawa wanafunzi wa kwanza hawakufanya hivyo. Walikuwa wameitikia wito wa Roho Mtakatifu katika mahubiri ya Yohana Mbatizaji. Sasa waliitambua sauti ya Mwalimu wa mbinguni. Maneno ya Yesu yalikuwa yamejaa upya, ukweli na uzuri kwao. Nuru ya kimbingu ilimwagwa kwenye mafundisho ya Maandiko ya Agano la Kale. Mada zile zenye mitazamo mingi-mingi zilisimama zikiwa katika nuru mpya." — *The Desire of Ages,* pp. 138, 139.

**b. Wanafunzi wa kwanza walifanya nini mara baada ya kukutana na yesu? Yohana 1:41, 42.**

---

---

---

"Andrea alitafuta kueneza furaha iliyokuwa imejaza moyo wake. Alienda kumtafuta ndugu yake Simoni, akapaza sauti akisema, „Tumemwona Masihi." Simoni hakusubiri hata kwa sekunde moja. Naye pia alikuwa amesikia mahubiri ya Yohana Mbatizaji, na aliharakisha kwenda kwa Mwokozi. "— *Ibid*, p.139.

## 4. KUVUNJA UBAGUZI — 1/8 (Jtano)

a. **Eleza kilichotokea Yesu alipomwalika mwanafunzi mwingine amfuate. Yohana 1:43–45.**

“Filipo alitii ile amri, na moja kwa moja akawa mtenda-kazi kwa ajili ya Kristo. Filipo alimwita Nathanaeli. ” — *The Desire of Ages,* p. 139.

b. **Tunaweza kujifunza nini kutokana na jinsi Kristo alivyoweza kushinda kusitasita kwa Nathanaeli? Yohana 1:46–49.**

“Nathanaeli alimtazama Yesu, akafadhaika. Je, mtu huyu, mwenye alama za umaskini na uchovu, aweza kuwa Masihi? Lakini Nathanaeli hakuweza kuamua kumkataa Yesu, maana ujumbe wa Yohana ulikuwa umeleta usadikisho katika moyo wake.

“Wakati huu Filipo alipomwita, Nathanaeli alikuwa amejitenga katika eneo tulivu lenye miti akitafakari juu ya tangazo la Yohana na unabii unaomhusu Masihi. Aliomba kwamba ikiwa yule aliyesemwa na Yohana ndiye mkombozi, ijulishwe kwake, na Roho Mtakatifu alikuja juu yake akimletea uhakika kwamba Mungu alikuwa amewajilia watu wake na kuinua pembe ya wokovu……

“Yesu akajibu, akamwambia, Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwapo chini ya mtini nilikuona.”

“Ilikuwa imetosha. Roho wa mbinguni aliyekuwa amemshuhudia Nathanaeli katika maombi yake ya faragha chini ya mtini sasa alisema naye katika maneno ya Yesu. Ingawa katika mashaka, na akikubali kwa namna fulani mawazo yake potofu ya kabla, Nathanaeli alikuwa amekuja kwa Kristo akiwa na hamu ya dhati ya kutaka ukweli, na sasa hitaji lake lilikuwa limejibiwa. Imani yake ilienda mbele zaidi ya ile ya yule aliyekuwa amemleta kwa Yesu. Alijibu na kusema, ”Rabi, wewe u Mwana wa Mungu, ndiwe Mfalme wa Israeli.”

“Ikiwa Nathanaeli angelitegemea uongozi wa marabi, asingelimwona Yesu kamwe. Ilikuwa ni kwa kuona na kuamua yeye mwenyewe ndipo alipopata kuwa mwanafunzi. Hivyo ndivyo ilivyo kwa wengi leo ambao wana mawazo yasiyo sahihi ambayo yanawashikilia mbali na wema. Je, kungekuwa na tofauti kiasi gani ikiwa wao wenyewe wangefuata wito kwamba ”njoo uone”!

“Wakati watu wanategemea kuongozwa na mamlaka za wanadamu, hakuna hata mmoja atakayefikia maarifa yaokoayo ya ukweli. Kama Nathanaeli, tunahitaji kujifunza neno la Mungu kwa ajili yetu wenyewe, na kuomba kuangaziwa na Roho Mtakatifu. Yeye aliyemwona Nathanaeli chini ya mti wa mtini atatuona hata sisi katika maeneo yetu ya faragha ya maombi. Malaika kutoka katika ulimwengu wa nuru wako karibu na wale ambao kwa unyenyekevu wanatafuta uongozi wa mbinguni.” — *Ibid.,* pp. 139 –140.

## 5. MBINGUNI WAZI — 1/9 (Alham)

a. Kristo alimwahidi nini Nathanaeli — na kwa nini? Yohana 1:50, 51.

---

---

[Yohana 1:50,51 imenukuliwa.]"Hapa ni kama Kristo anasema, kwenye kingo za Yordani mbingu zilifunguka, na Roho alishuka kama hua juu yangu. Tukio lile lilikuwa ishara tu kwamba mimi ni Mwana wa Mungu. Mkiniamini hivyo, imani yenu itaimarishwa. Mtaona kwamba mbingu zimefunguliwa, na hazitafungwa kamwe. Nimezifungua kwenu. Malaika wa Mungu wanapanda, wakipeleka kwa Baba maombi ya wenye kuhitaji na waliochoka, na wanashuka, wakileta baraka na tumaini, ujasiri, msaada, na uzima, kwa wana wa wanadamu. " — *The Desire of Ages,* pp. 142, 143.

b. Nini kinatokea tunapompokea Kristo? Yohana 4:14; Ufunuo 22:17.

---

---

"Wakati mtu anapokuwa amepokea ukweli kwa kuupenda, ataufanya udhihirike katika kuirekebisha tabia yake na toni ya sauti yake. Anawafanya na wengine wajue kile ambacho hata yeye amekisikia, kukiona, na kilichotolewa kwa neno la uzima, ili ya kwamba na wengine washiriki naye katika kumjua Kristo. Ushuhuda wake, utokao katika midomo iliyoguswa na kaa la moto lililotwaliwa kutoka madhabahuni, ni ukweli kwa moyo upokeao, na hufanya kazi ya utakaso wa tabia.

"Mungu aweza kufikia kusudi lake la kuwaokoa wadhambi bila msaada wetu; lakini ili tukuze tabia kama ya Kristo, lazima tushiriki katika kazi yake. Ili tuingie katika furaha yake, - furaha ya kuziona roho zikikombolewa kwa kafara ya Yesu – lazima tushiriki katika kazi zake kwa ajili ya ukombozi wao. "— *Ibid.*, p.142.

## 6. MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI — 1/10 (Ijuma)

1. Kwa nini Yohana Mbatizaji aliitwa jangwani?
2. Je, tunapaswa kutumiaje mtindo wa maisha wa Yohana Mbatizaji kwa maisha yetu wenyewe?
3. Tunaweza kujifunza nini kutoka kwa Yohana na Andrea walipokutana na Yesu?
4. Tunawezaje kutiwa moyo na tangazo la awali la Nathanaeli?
5. Ni nini kinachoonyesha kama imani yangu katika Kristo ni ya kweli au la?

Sabato, Januari 18, 2025

**Somo la 3**

# Harusi ya Kana

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Lo lote atakalowaambia, fanyeni" (Yohana 2:5, sehemu ya mwisho).

**Inapendekezwa kusoma:** *The Desire of Ages,* pp. 144–153; *Messages to Young People,* pp. 403–418.

"Yesu aliianza kazi yake ya matengenezo kwa kuja katika huruma ya karibu na wanadamu." — *The Desire of Ages,* p. 150.

## 1. MWANZO WA UTUME WA KRISTO — 1/12 (Jpil)

a. Yesu alianzia wapi utume wake duniani? Yohana 2:1, 2.

"Yesu hakuanza kazi yake kwa matendo makubwa mbele ya Sanhedrin kule Yerusalemu. Uwezo wake ulipelekwa katika kusanyiko la nyumbani katika kijiji kidogo kilichoko kule Galilaya ili kuongezea katika furaha ya karamu ya arusi. Hivyo ndivyo alivyoonyesha huruma kwa watu, na hamu yake ya kutumika kwa ajili ya furaja yao. Katika jangwa la majaribu Yeye mwenyewe alikuwa amekunywa kikombe cha huzuni. Hapa alikuja kuwapa watu kikombe cha baraka, kwa kutoa kwake kwa kuheshimu mahusiano katika maisha ya wanadamu." — *The Desire of Ages,* p. 144.

b. Nini kilitokea kabla ya mwisho wa karamu ya harusi? Yohana 2:3.

"[Mariamu] alitamani Yesu athibitishie watu wale kwamba alikuwa Aliyeheshimiwa na Mungu. Alitamani kuwe na fursa ya Yeye kufanya mwujiza mbele yao.

"Ilikuwa desturi ya wakati huo kwa sherehe za ndoa kuendelea kwa siku kadhaa. Katika tukio hili, divai iliisha kabla ya sherehe kufika mwisho. Hali hii ilisababisha wasiwasi na masikitiko makubwa. Ilikuwa si kawaida kukosekana divai katika matukio ya sherehe, na kukosekana kwake kungeashiria utovu wa ukarimu. " – *Ibid.*, p.145,146.

## 2. KRISTO NA MAMA YAKE



a. Mama yake Kristo alisema nini, na jibu lake lilikuwa nini? Yohana 2:3, 4.

“[Yohana 2:4 imenukuliwa]Jibu hili, lililo la ghafla kama lionekanavyo kwetu, lilionyesha kutojali na utovu wa adabu. Namna ile Yesu alivyosema kwa mama yake ilikuwa sahihi kulingana na desturi za Asia Mashariki. Usemi huo ulitumika kwa watu ambao walikuwa wanaonyeshwa kuheshimiwa. Kila tendo lililotendwa katika maisha ya Yesu duniani lilikuwa linakubaliana na amri aliyokuwa ametoa isemayo, „Waheshimu baba yako na mama yako.” Kutoka 20:12. Alipokuwa msalabani, katika tendo lake la mwisho la kuonyesha huruma kwa mama yake, Yesu alizungumza na mama yake kwa namna hiyo hiyo, wakati alipomkabidhi uangalizi wa mwanafunzi yule aliyempenda sana. Katika matukio yote haya mawili ya arusini na msalabani, upendo ulioonyeshwa katika sauti na mwonekano na adabu vilionyesha tafsiri ya maneno yake. ” — *The Desire of Ages,* p. 146.

b. Mama yake Kristo aliwaambia nini watumishi — na maneno hayo yanatuhusuje sisi leo? Yohana 2:5.

“Wafuasi [wa kristo] wanapaswa kuwa na nguvu zaidi na zaidi katika kuitangaza Kweli kadiri wanavyosogea kwenye utimilifu wa imani na upendo kwa ndugu zao. Mungu ametoa usaidizi wa mbingu kwa dharura zote ambazo rasilimali zetu za kibinadamu haziwezi kumudu. Yeye hutoa Roho Mtakatifu kusaidia katika kila shida, kuimarisha tumaini letu na uhakika, kuangaza akili zetu na kusafisha mioyo yetu. Anamaanisha kwamba vifaa vya kutosha vitatolewa kwa ajili ya kufanya kazi nje ya mipango yake. Nakuagiza utafute ushauri kwa Mungu. Mtafuteni kwa moyo wote, na „lolote awaambialo, fanyeni.” Yohana 2:5.”— *Testimonies for the Church,* vol. 6, pp. 414, 415.

c. Yesu alimwambia mtumishi kwenye harusi afanye nini? Yohana 2:6–8.

“Kando ya mlango kulikuwa na mabalasi makubwa sita ya mawe, na Yesu akawaambia mahudumu wale wayajaze maji. Ikafanyika hivyo. Kisha wakati divai ilipotakiwa ili kutumika, aliwaambia, „Sasa tekeni, mkampelekee mkuu wa meza.” Badala ya maji yaliyokuwa yamejazwa, kulimiminika divai” — *The Desire of Ages,* p. 148.

## 3. DIVAI YA KRISTO



### a. Divai ilipotolewa, mkuu wa karamu alijibuje? Yohana 2:9,10.

"Si mkuu wa meza wala wageni waalikwa waliojua kwamba divai ilikuwa imepwelea. Alipoonja hii divai iliyoletwa na wahudumu, mkuu wa meza aliona ikiwa njema kuliko nyingine yoyote aliyokuwa amepata kunywa kabla, na ikiwa tofauti sana na ile iliyokuwa imetolewa mwanzoni mwa sherehe ile. " — *The Desire of Ages,* p. 148.

### b. Kristo alitoa divai ya aina gani? Isaya 65:8.

"Ile divai ambayo Kristo alitoa wakati wa sherehe, na ile aliyotoa kwa wanafunzi wake kama ishara ya damu yake, ilikuwa ni juisi safi ya zabibu. Nabii Isaya anairejea anaposema kuhusu divai mpya "katika kichala," na anasema, "Usikiharibu kwa maana mna baraka ndani yake." Isaya 65:8. . . . .

"Divai isiyochachushwa aliyotoa kwa wageni wa arusi ilikuwa kinywaji kizuri cha kuburudisha. Kazi yake ilikuwa ni kuleta ladha inayokubaliana na hamu inayozingatia afya. "— *Ibid.*, p.149.

### c. Maandiko yanasema nini kuhusu divai iliyochacha? Mithali 20:1; 23:29–35.

"Ni Kristo ambaye aliwapa onyo Israeli katika Agano la Kale akisema, "Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi; Na akosaye kwa vitu hivyo hana hekima." Methali. 20:1. Hata Yeye hakutoa kinywaji kama hicho. Shetani anawajaribu watu katika kutimiza hamu zao kwa kile kinachoharibu akili na kuchafua ufahamu wa kiroho, lakini Yesu anatufundisha kutawala tamaa zetu. Maisha yake yote yalikuwa kielelezo cha kujikana. Ili kuvunja nguvu za hamu ya kula na kunywa, aliumia katika jaribu kali mno ambalo hakuna mwanadamu anayeweza kustahimili jaribu zaidi ya hilo. Ni Kristo aliyeagiza kwamba Yohana Mbatizaji asinywe divai wala kileo. Ni Yeye pia aliyetaka kujitawala huko huko kwa mke wa Manoa. Na alitamka laana kwa mtu yeyote ambaye angeweka chupa katika midomo ya jirani yake. Kristo hakujipinga katika mafundisho yake mwenyewe." — Ibid.

## 4. MFANO WA KRISTO KWENYE MIKUTANO YA KIJAMII 1/15 (Jtano)

**a. Ni malengo gani yalifikiwa kupitia uwepo wa Kristo na muujiza Wake kwenye karamu ya harusi, hata kwetu sisi leo? Yohana 2:11.**

---

“Kristo alijua mambo yote; Alitazama chini enzi hadi wakati wetu, na akaona nini ingekuwa hali ya jamii katika mwisho wa historia ya ulimwengu. Aliona maelfu kwa maelfu wakiangamia kwa matumizi ya divai na vileo vikali. Ulimwengu ungekuja polepole katika hali ile ile kama ilivyokuwa siku za kabla ya gharika. Lakini mbingu imeinua ishara ya hatari, ili watu wapate maonyo, na kushirikiana na Mungu kwa ajili ya kujilinda wao wenyewe. Ametupa vielelezo vya kujizuia kabisa, na kutoa maagizo ambayo, yakifuatwa, yatatokeza kuumbwa na kuhifadhiwa kwa nguvu, ustadi, na ubora wa watoto wetu.” — *The Signs of the Times,* Aprili 16, 1896.

**b. Elezea aina ya mtazamo wenye kuburudisha ambao Kristo alionyesha katika huduma Yake yote. Mathayo 11:29.**

---

“Yesu aliianza kazi yake ya matengenezo kwa kuja katika huruma ya karibu na wanadamu. Wakati alionyesha heshima kubwa kwa sheria ya Mungu, alikemea uchaji-Mungu wa kujionyesha wa Mafarisayo, na alijaribi kuwafanya watu wawe huru pasipo kufungwa na taratibu zisizo maana ambazo zilikuwa zimewafunga. Alikuwa anajitahidi kuvunja vizuizi vilivyotenganisha matabaka tofauti-tofauti ya jamii, ili kwamba awalete watu pamoja kama watoto wa jamaa moja. Kuhudhuria kwake kwenye sherehe ya arusi kulipangwa kama hatua ya kuelekea katika kutekeleza nia hii. ” — *The Desire of Ages*, p. 150.

“Yesu alikemea ubinafsi katika aina zake zote, lakini alikuwa na hali ya kuhusiana na wengine. Alikubali ukarimu wa watu wa matabaka yote, akitembelea nyumba (151) za matajiri na maskini, waliosoma na wasio na kisomo, na akitafuta kuinua mawazo yao kutoka katika mambo ya kawaida ya mahali walipokuwa kwenda katika mambo ya kiroho ya milele. Hakutoa kibali cha kufanya ufujaji, na mwenendo wake haukuwa na uvuli wa kukosa staha; lakini alipata raha katika matukio ya furaha isiyo na hatia. Ndoa ya Kiyahudi ilikuwa tukio la kuvutia, na furaha ya ndoa ile haikuwa mbaya kwa Mwana wa Adamu. Kwa kuhudhuria sherehe hii, Yesu aliheshimu ndoa kama jambo lililowekwa na Mungu” — *Ibid.*, pp. 150, 151.

## 5. UHUSIANO MZURI WA KIJAMII — 1/16 (Alham)

a. **Tunapaswa kujifunza nini kutokana na kielelezo cha Kristo ambacho kilimtofautisha na watawala wa kidini wa siku zake? Mithali 18:24.**

---

“Huduma ya Yesu ilikuwa tofauti kabisa na mtazamo wa wazee wa Kiyahudi. Heshima yao kwa desturi za mazoea ilikuwa imeharibu uhuru halisi wote wa mawazo na matendo. Waliishi katika uchafu wa kutisha wa kudumu. Wakikwepa kukutana na „walio najisi,” walidumu kujitenga, si tu na Mataifa, bali na hata walio wengi miongoni mwa watu wa taifa lao, wakitafuta kwamba wasinufaike nao kwa lolote wala wasipate urafiki kwao. Kwa kuzama katika mambo haya wakati wote, walikuwa wamepotosha mawazo yao na kufanya upeo wa maisha yao kuwa finyu. Kielelezo chao kilifundisha kujipenda na kukosa uvumilivu miongoni mwa matabaka yote ya watu.” — *The Desire of Ages,* p. 150.

b. **Je, lengo letu linapaswa kuwa nini katika maingiliano yote ya kijamii? Mithali 11:30.**

---

“Tunaweza kudhihirisha uangalifu mdogo kwa maneno ya kirafiki na sura za kupendeza, ambazo zitaakisiwa kwetu tena. Wakristo wasio na mawazo hudhihirisha kwa kutowajali wengine kwamba wao si katika muungano na Kristo. Haiwezekani kuwa katika muungano na Kristo na bado tusiwe na fadhili kwa wengine na kusahau haki zao.

“Sote tunapaswa kuwa mashahidi wa Yesu. Nguvu ya kijamii, iliyotakaswa kwa neema ya Kristo, lazima iboreshwe katika kuzileta roho kwa Mwokozi. Acha ulimwengu uone kwamba hatujishughulishi kwa ubinafsi na masilahi yetu wenyewe, bali kwamba tunatamani wengine washiriki baraka na mapendeleo yetu. Waone kwamba dini yetu haitufanyi tusihurumike au kutulazimisha. Wacha wote wanaodai kuwa wamempata Kristo wahudumu kama alivyofanya kwa faida ya wanadamu. Hatupaswi kamwe kuupa ulimwengu maoni ya uwongo kwamba Wakristo ni watu wenye huzuni na wasio na furaha.” — *The Adventist Home,* p. 428.

## 6. MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI — 1/17 (Ijumaa)

1. Elezea matunda ya kiroho yanayoletwa na muujiza wa Kristo huko Kana.
2. Elezea uhusiano kati ya Kristo na mama yake.
3. Kwa nini gavana wa sikukuu alionyesha mshangao?
4. Ni aina gani ya divai inayofananisha ipasavyo damu ya Kristo?
5. Kwenye makusanyiko ya kijamii, tunapaswa kukumbuka nini kutokana na mfano wa Yesu?

Sabato, Januari 25, 2025

**Somo la 4**

# Yesu Hekaluni

**FUNGU LA KUKARIRI:** ”Lakini Bwana yumo ndani ya hekalu lake takatifu, dunia yote na inyamaze kimya mbele zake” (Habakuki 2:20).

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 5, pp. 491–500.

“Maeneo ya kanisa yanapaswa kuwekezwa kwa kicho kitakatifu. ”—*Testimonies for the Church,* vol. 5, p. 494.

## 1. KUNAJISIWA KWA HEKALU — 1/19 (Jpil)

**a. Eleza hali iliyokuwa katika hekalu la Yerusalemu mwanzoni mwa huduma ya hadhara ya Kristo. Yohana 2:13, 14.**

---

“Kila Myahudi alitakiwa kulipa nusu shekel kila mwaka kama ”ukombozi kwa ajili ya roho yake” Licha ya hii, matoleo makubwa mengine yaliletwa kama sadaka za hiari, ili kuwekwa katika hazina ya hekalu. Na ilitakiwa kwamba sarafu zote za kigeni zibadilishwe katika sarafu iliyoitwa shekeli ya hekalu, ambayo ilipokelewa kwa ajili ya huduma za patakatifu. Kazi hii ya kubadilisha fedha ilitoa fursa ya kufanya udanganyifu na kutoza bei kubwa, na hali hiyo ilikua na kuwa biashara haramu, iliyokuwa chanzo cha mapato cha makuhani.

“Waendeshaji wa biashara hizo waliuza wanyama kwa bei ya juu sana, na waligawanya faida kwa makuhani na wakuu pia, ambao kama matokeo yake walijitajirisha kwa kuwanyonya watu. ” — *The Desire of Ages,* p. 155.

**b. Je, hii iliathiri vipi huduma za hekalu? Ezekieli 22:26 (sehemu ya mwisho).**

---

“Idadi kubwa ya kafara ilitolewa wakati wa Pasaka, na mauzo pale hekaluni yalikuwa makubwa sana. Matokeo ya mchanganyiko wa fujo ya sauti katika uuzaji huu ulifanya eneo lile liwe kama mnada wa mifugo wenye kelele badala ya kuwa hekalu takatifu la Mungu. Kulikuwa kunasikika sauti za majadiliano ya bei, sauti za milio ya ng’ombe, miguno ya kondoo, milio ya njiwa, vikiwa vimechanganyika na mlio wa sarafu na sauti za hasira za watu wanaoshindwa kukubaliana. Kwa hiyo mchanganyiko ulikuwa mkubwa sana kiasi cha kuwasumbua wanaoabudu, na maneno yaliyoelekezwa kwake Aliye Juu yalifunikwa na kelele zilizovamia hekalu.”—Ibid.

**a. Je, Mungu huzingatiaje mahali ambapo Yeye hudhihirisha uwepo Wake—na ni maagizo gani ya kwanza katika Mlima Sinai? Kutoka 3:1–5; 19:12, 13.**

---

"Wakati Bwana aliposhuka kwenye Mlima Sinai, eneo lile lilitakasika kwa uwepo wake..... Hivyo somo lilitolewa kwamba mahali popote ambapo Mungu anadhihirisha uwepo wake, hiyo sehemu ni takatifu." — *The Desire of Ages,* pp. 155, 156.

**b. Kristo aliitikiaje kunajisiwa kwa hekalu? Yohana 2:15, 16.**

---

"Yesu alipoingia hekaluni, aliangalia mandhari yote. Aliona miamala isiyo ya haki. Aliona shida za maskini, ambao walidhani kwamba pasipo kumwaga damu hakuna msamaha wa dhambi. Aliona ukumbi wa nje wa hakalu lake ukiwa umebadilishwa kuwa mahali pa biashara isiyo takatifu. Eneo takatifu lilikuwa limefanywa kuwa kituo kikubwa cha kuuzia na kubadilishia. " — *Ibid.,* p. 157.

"Akishuka katika ngazi taratibu, aliinua mjeledi wa kamba zilizofungwa pamoja na kuwaendea, akiwataka wanaofanya biashara waondoke katika viwanja vya hekalu. Akiwa na ushujaa na hasira ambazo hajawahi kuonyesha kabla, alisukuma na kupindua-pindua meza za wale wanaobadili pesa. Sarafu zinadondoka, zikitoa sauti kwenye sakafu ya marumaru. Hakuna anayediriki kuhoji mamlaka yake. Hakuna anayezuia na kutaka biashara iendelee. Yesu hawachapi kwa ule mjeledi wa kamba, lakini mkononi mwake mjeledi ule ulitisha kama upanga uwakao. Maofisa wa hekalu, makuhani, wachuuzi na wafanya biashara ya ng'ombe, wakiwa na kondoo na punda wao, wanakimbia kutoka pale, wakiwa na wazo moja la kuikimbia hukumu ya uwepo wa Yesu." — *Ibid.,* p. 158.

**c. Tendo la Kristo la kutakasa hekalu lilimaanisha nini? Malaki 3:1–3.**

---

"Vile viwanja vya hekalu la Yerusalemu", vilivyojawa na fujo za biashara isiyo takatifu, viliwakilisha kwa usahihi kabisa hekalu la moyo, ambalo limechafuliwa na uwepo wa hisia za tamaa na mawazo yasiyo na utakatifu. Katika kule kusafisha hekalu kutokana na wauzaji na wanunuzi wa kiulimwengu, Yesu alitangaza kazi yake ya kusafisha moyo kwa kuondoa uchafu wa dhambi, - kutokana na tamaa ya mambo ya kidunia, ubinafsi, tabia za uovu, ambazo zinaharibu roho." – *Ibid.*, p.161.

## 3. UWEPO WA MUNGU — 1/21 (Jnne)

**a. Kusudi la awali la Mungu lilikuwa nini katika kuanzisha patakatifu pake kati ya watu wake? Kutoka 25:8.**

"Kanisa lile ambalo lilijengwa ili kuwa makao ya Mungu lilipangwa kuwa kama somo kwa Israeli na kwa ulimwengu. Tangu milele ilikuwa kusudi la Mungu kwamba kila kiumbe, tangu serafi mtakatifu na mwenye utukufu mpaka mwanadamu, awe ni hekalu kwa ajili ya makao ya Mwumbaji. " — *The Desire of Ages,* p. 161.

**b. Kwa nini waumini wanarejelewa kama hekalu la Mungu—na ni kwa jinsi gani tunapaswa kudumisha utakatifu wa hekalu hili kwa moyo wote? 1 Wakorintho 3:16, 17; Isaya 57:15.**

"Kwa sababu ya dhambi, mwanadamu alikoma kuwa hekalu la Mungu. Ukiwa umetiwa giza na kuchafuliwa na uovu, moyo wa mwanadamu haukuweza tena kufunua utukufu wa Mungu. Lakini kwa Mwana wa Mungu kufanyika mwanadamu, kusudi la mbingu linatimizwa. Mungu anakaa ndani ya mwanadamu, na kwa njia ya neema iokoayo moyo wa mwanadamu unakuwa hekalu lake"—Ibid.

"Ikiwa tunaamini kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia, 'imewapasa ninyi kuwa watu wa namna gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa?'

"Kila nafsi inayoamini Kweli itakuwa na matendo yanayolingana. Wote watakuwa na bidii na taadhima, na bila kuchoka katika juhudi zao za kuleta roho kwa Kristo. Iwapo Kweli itawekwa ndani kabisa ndani ya nafsi zao, basi watatafuta kuipanda katika mioyo ya wengine. Ukweli umehifadhiwa sana katika nyua ya nje. Ilete ndani ya hekalu la ndani la roho, na iweke enzi moyoni, na iruhusu itawale maisha. Neno la Mungu linapaswa kuchunguzwa na kutiiwa, ndipo moyo utapata pumziko na amani na furaha, na matarajio yataelekea mbinguni; lakini Ukweli unapowekwa kando na uzima, katika ua wa nje, moyo haupati joto au hauwashwi na moto unaowaka wa wema wa Mungu.

"Dini ya Yesu, kwa wengi, imehifadhiwa kwa siku fulani, au matukio fulani, na wakati mwingine inawekwa kando na kupuuzwa. Kanuni ya kudumu ya Ukweli si kwa masaa machache tu siku ya Sabato, au kwa matendo machache ya hisani/huduma, bali inapaswa kuletwa ndani ya moyo, ikisafisha na kuitakasa tabia." — *Testimonies for the Church*, vol 5, p. 547.

## 4. UTAKASO WA HEKALU LILILO HAI — 1/22 (Jtan)

**a. Ni nini lazima tutambue kuhusu hali yetu ya kutokuwa na uwezo katika kutafuta kutakasa hekalu? Yeremia 2:22; Ayubu 14:4.**

---

---

"Hakuna mtu ambaye anaweza yeye mwenyewe kuondoa mkusanyiko wa maovu ambao umetawala moyo. " — *The Desire of Ages,* p. 161.

**b. Je, ni siri gani ya kuweza kusimama mbele za Mungu mtakatifu kwa moyo safi? Ezekieli 36:25–27; Zekaria 3:3–5.**

---

---

"Yakobo alikuwa na hatia ya dhambi kubwa iliyotokana na kibaya alichomtendea Esau; lakini alikuwa ametubu. Uovu wake ulikuwa umesamehewa, na alikuwa ameoshwa dhambi yake; kwa hiyo angestahimili ufunuo wa kuwepo kwa Mungu. Lakini kila mahali ambapo watu walikuja mbele za Mungu wakiwa na uovu kwa makusudi, waliangamizwa. Wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili waovu watateketezwa „kwa pumzi ya kinywa chake," na kuangamizwa kwa „ufunuo wa kuwapo kwake." 2 Wathesalonike 2:8. Nuru ya utukufu wa Mungu, ambayo inaleta uzima kwa wenye haki, itawaua waovu.

"Mnamo wakati wa Yohana Mbatizaji, Kristo alikuwa atokee kama mfunuaji wa tabia ya Mungu. Uwepo wake tu ungewadhihirishia watu dhambi yao. Ni pale tu ambapo wangekuwa tayari kuoshwa dhambi zao ndipo wangeweza kuingia katika mjumuiko pamoja naye. Ni wenye moyo safi tu ambao wangekuwa naye katika uwepo wake. " — *Ibid.*, p. 108.

"Kristo pekee ndiye anaweza kulisafisha hekalu la moyo. Lakini hatalazimisha kuingia. Haji moyoni kama alivyofanya alipoingia katika hekalu la zamani; bali anasema, "Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake." Ufunuo 3:20. Hatakuja kwa siku moja pekee; maana anasema, "Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea; . . . nao watakuwa watu wangu." "Atayakanyaga maovu yetu; nawe utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari." 2Wakorintho 6:16; Mika 7:19. Uwepo wake utasafisha na kutakasa moyo, ili upate kuwa hekalu takatifu kwa Bwana, na kuwa "maskani ya Mungu katika Roho." Waefeso 2:21, 22. " — *Ibid.,* pp. 161, 162.

"Wakati Yesu akihudumu katika patakatifu pa huko juu, bado ni mhudumu wa kanisa duniani ." — *Ibid.*, p. 166.

## 5. KUTAKASA HEKALU LEO — 1/23 (Alhamis)

**a. Je, Mungu anawawajibishaje viongozi wa watu wake ili kushikilia kwa bidii utakatifu wa nyumba yake? Habakuki 2:20; Ezekieli 44:23.**

---

"Viwanja vya hekalu la Mungu vingechukuliwa kama vitakatifu. Lakini katika kutafuta faida, yote haya hayakuonwa.

"Makuhani na wakuu waliitwa wawakilishi wa Mungu kwa taifa lao; iliwapasa kusahihisha matumizi mabaya ya viwanja vya hekalu. Iliwapasa kuonyesha kielelezo cha uadilifu na huruma. " — *The Desire of Ages,* p. 156.

"Ni kweli kabisa kwamba heshima ndani ya nyumba ya Bwana imekaribia kutoweka. Vitu vitakatifu havitambuliwi na wala mahali Patakatifu hapatambuliwi; Vitakatifu na vilivyotukuka havithaminiwi. Je! Hakuna sababu inayopelekea kukosekana kwa kicho na heshima yenye bidii na dhati mbele za Mungu katika familia zetu? Je, si kwamba viwango vya juu vya dini vimeachwa kuburuzika mavumbini? Mungu alitoa Sheria za utaratibu, kamilifu na halisi, kwa watu Wake wa kale. Je tabia Yake imebadilika? Je! Yeye si Mungu Mkuu na hodari anayetawala mbingu na nchi? Je! Haitakuwa vizuri kwetu sisi kusoma mara nyingi kadri tuwezavyo miongozo iliyotolewa na Mungu Mwenyewe kwa Waebrania, ili sisi ambao tuna nuru ile ya Kweli na tukufu inayoangaza juu yetu tuweze kuiga kicho kama chaokatika nyumba Yake? Tuna sababu nyingi za kuwa na bidii, na kujitoa wakfu kwelikweli katika ibada ya Mungu." — *Testimonies for the Church,* vol. 5, pp. 495, 496.

**b. Elezea ushindi muhimu unaopatikana kwa nguvu za Kristo. Mathayo 5:8; 1 Yohana 3:1–3.**

---

"Natoa wito kwa kila mtu anayedai kuwa mwana wa mungu kamwe asisahau ukweli huu mkuu, kwamba tunahitaji Roho wa Mungu ndani yetu ili kufikia mbingu, na kazi ya Kristo bila sisi ili kutupa jina urithi usioweza kufa. " — *Testimonies to Ministers,* p. 442.

## 6. MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI — 1/24 (Ijumaa)

1. Ni akina nani walikuwa viongozi wa biashara chafu hekaluni?
2. Je,mtu yeyote anayekuja mbele za Mungu anapaswa kuwa na mtazamo gani?
3. Eleza umuhimu wa kiroho ambao hekalu la Yerusalemu lilipaswa kuwa nao.
4. Kristo alitangaza nini katika kutakasa hekalu?
5. Ni kwa jinsi gani moyo wetu wenye kasoro unaweza kusafishwa?

# Sadaka za sabato ya kwanza

Sabato, Februari 1, 2025

## Msaada wa Maafa Ulimwenguni



Hapana shaka kwamba vita, uvumi wa vita, ajari zenye kuogofya, ukame, mafuriko, vimbunga, matetemeko ya ardhi, moto, na magonjwa ya kuambukiza yanaongezeka ulimwenguni pote kwa kasi kubwa—yote hayo yakitimizwa unabii wa Biblia tunaojifunza. Bila shaka, katika misiba hiyo yote, tunaweza kutambua waziwazi nyayo za Mungu anayemkaribia. Maelfu mengi ya watu wanateseka sana kutokana na magumu hayo makubwa, wakitaka msaada wa aina mbalimbali kutoka kwa mabalozi wa Yesu Kristo ili kutia zeri ya uponyaji ya Gileadi.

Katika hali hizi chungu nzima, Idara ya Ustawi ya GC imeshiriki baraka zinazotolewa na hazina yetu kupitia matoleo yaliyotumwa na ninyi, ndugu zetu duniani kote. Haya yanatumwa kwa njia ya kibinafsi na mahususi ili kukidhi mahitaji, na pia kupitia Matoleo ya Sabato ya Kwanza. Ndugu wapendwa, sadaka zenu zimetumika

kama makazi kwa wale waliopoteza makazi yao katika misiba ya asili; wametoa chakula kwa mamia ya familia na kuwatunza mayatima na wajane, wakiwapa riziki na msaada. Sadaka hizi pia zimesaidia wazazi kupata mbegu za kupanda na kulisha familia zao au kuanzisha biashara ndogo ndogo ili watu wasiohesabika wa imani yetu wanaweza kuwa na chanzo cha mapato na kazi ambayo vinginevyo isingewezekana kwao

Namshukuru Mungu kwamba katika nyakati hizi za majaribu, wengi wameguswa kuweka michango yao kwenye madhabahu ya Bwana. Kwa niaba ya wale wanaohudumiwa, tunakushukuru sana!

Hata hivyo, mahitaji hayakomi—kinyume chake, yanaongezeka zaidi kila siku, kwa hiyo ukarimu wako unasaidia sana.

“Msalaba wa Kristo unasihi wema wa kila mfuasi wa Mwokozi aliyebarikiwa. Kanuni iliyoonyeshwa hapo ni  kutoa. Hili, linalofanywa kwa hisani halisi na matendo mema, nitunda la kweli la maisha ya Kikristo.”— *Counsels on Stewardship*, p. 14.

Leo, unapotoa sadaka yako maalum kwa ajili ya Sabato ya kwanza, tafadhali fanya yote uwezayo kumheshimu Mungu. Iwe na kidogo

au mengi, wote wanaweza kufanya bora zaidi. Kutokana na jumla ya upendo huu wa pamoja, tutaendelea kusambaza baraka kwa ndugu zetu kote ulimwenguni. „Yeye anayewapa wahitaji huwabariki wengine, na anajibariki kwa kiwango kikubwa zaidi” (Ibid., p. 13). Mungu akubariki sana!

*GC Idara ya Ustawi*

Sabato, Februari 1, 2025

**Somo la 5**

# Yesu na Nikodemo

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu" (Yohana 3:3).

**Inapendekezwa kusoma:** *Steps to Christ,* pp. 67–75.

"Chemchemi ya moyo isafishwe kabla ya vijito kuwa safi. Yeye anayejaribu kwenda mbinguni kwa matendo yake ya kushika sheria anajaribu kufanya lisilowezekana. " — *The Desire of Ages*, p. 172.

## 1. MTU MAARUFU AMTAFUTA YESU — 1/26 (jpil)

**a. Nikodemo alikuwa nani, na alizingatiwaje machoni pa watu? Yohana 3:1, 10.**

"Nikodemo alikuwa na nafasi ya juu ya kutumainiwa katika taifa la Uyahudi. Alikuwa mtualiyeelimika sana, na alikuwa na vipaji ambavyo si vya tabia ya kawaida, na alikuwa mjumbe wa heshima katika baraza la taifa. Ingawa alikuwa tajiri, aliyesoma, na mwenye kuheshimiwa, alikuwa amevutiwa na huyu Mnazareti mnyenyekevu." — *The Desire of Ages,* p.167.

"Alikuwa Farisayo hasa, na alijivunia matendo yake mema. Alikuwa mtu wa kutukuzwa sana kwa ukarimu wake na utayari wa kuwezesha huduma za hekalu, na alifikiri yuko salama mbele za Mungu. " — *Ibid.*, p.171.

**b. Ni saa ngapi Nikodemo alienda kukutana na Yesu? Yohana 3:2 (sehemu ya kwanza).**

"Akitumia njia maalum ya kuulizia-ulizia kuhusu mahali Yesu anapopumzikia katika Mlima wa Mizeituni, alisubiri mpaka mji ulipokuwa kimya watu wakiwa wamelala, ndipo alipomtafuta. " — *Ibid.,* p. 168.

## 2. MAHOJIANO YA FARAGHA 1/27 (Jtatu)

**a. Ni nini kinaonyesha uelewa mzuri wa Yesu katika kumpokea mgeni wake saa za usiku sana? Zaburi 31:20, 21.**

---

---

"[Nicodemo] Alitamani sana ahojiane na Yesu, lakini aliogopa kumtafuta waziwazi. Ingekuwa jambo la kudhalilisha sana kwa mkuu wa Wayahudi kujisalimisha kwa mwalimu ambaye alikuwa bado anajulikana kidogo namna ile. Na ikiwa habari ya jambo kama hilo ingewafikia wajumbe wa Sanhedrin, lingemletea kudharauliwa na kushutumiwa. Aliazimia kufanya mahojiano ya siri, akitolea sababu kwamba ikiwa angeenda waziwazi, na wengine wangefuata mfano wake. " — *The Desire of Ages,* p. 168.

**b. Eleza jinsi Nikodemo alianza mahojiano yake na Yesu. Yohana 3:2.**

---

---

"Mbele ya uwepo wa Yesu, Nikodemo alikosa hali ya kujiamini kwa namna ambayo haikutarajiwa, ambayo aliamua kuificha kwa kutulia na kuwa na heshima. Alisema, „Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye." Kwa kuongea kuhusu vipawa maalum vya Kristo kama mwalimu, na kuhusu uwezo wake wa ajabu wa kutenda miujiza, alitumaini kwamba anaweka njia kwa ajili ya mahojiano yake. Maneno yake yalipangwa kuonyesha na kukaribisha hali ya kujiamini; lakini kumbe yalionyesha hasa kutokuamini. Hakukiri kwamba Yesu ni Masihi, bali kwamba ni mwalimu aliyetumwa kutoka kwa Mungu. " — Ibid.

**c. Je, Kristo alimshangaza Nikodemo kwa dhana gani ghafla? Yohana 3:3.**

---

---

"Badala ya kutambua maneno haya ya salamu, Yesu alimkazia macho huyo aliyesema, kama vile alikuwa anasoma moyo wake. Katika hekima yake isiyo mwisho pale alimwona mtu anayetafuta ukweli. Alijua lengo la ujio huu, na akiwa na hamu ya kuimarisha kwa kina imani iliyokuwa katika ufahamu wa msikilizaji wake huyu, alikuja kwenye kiini chenyewe, akisema wazi, lakini kwa upendo, „Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu." Yohana 3:3.

"Nikodemo alikuwa amekuja kwa Bwana akidhani ya kwamba atafanya naye majadiliano, lakini Yesu aliweka wazi kanuni za msingi za ukweli. " — *Ibid.* pp. 168 – 171.

**a. Je, Nikodemo aliitikiaje kile ambacho Kristo alisema alihitaji — na, kama yeye, kwa nini sote tunahitaji tukio la kuzaliwa upya? Yohana 3:4–8.**

"Stiari ya kuzaliwa upya iliyotumiwa na Yesu si kwamba ilikuwa haijulikani kabisa kwa Nikodemo. Waongofu waliotoka upaganini kuja katika imani ya Israeli walilinganishwa mara nyingi na watoto ambao wamezaliwa. Kwa hiyo lazima atakuwa alielewa kwamba maneno ya Kristo hayakuwa na maana ya moja kwa moja ya kawaida. Lakini kwa kuzaliwa kwake kama Mwisraeli alijiona kuwa na uhakika wa nafasi katika ufalme wa Mungu. Alifikiri kwamba hakuhitaji badiliko. Ndiyo sababu alishangazwa na maneno ya Mwokozi. Alisumbuliwa na hali ya meneno hayo kuhusishwa naye. Kiburi cha Farisayo kilikuwa kinapambana na hamu ya uaminifu ya kutafuta ukweli. Alishangaa kwamba ni kwa nini Kristo alimsema vile, pasipo kuheshimu nafasi yake kama mkuu katika Israeli.

"Akishangazwa na kushindwa kujitawala, alimjibu Kristo kwa maneno yaliyo kinyume, "Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee?" Kama walivyo wengi wengine pindi ukweli mkali ukatao unapoletwa mahali pake katika dhamiri zao, alidhihirisha ukweli kwamba mwanadamu kwa asili hapokei mambo ya Roho wa Mungu. Ndani yake hamna kitu kinachoitikia mambo ya kiroho; maana mambo ya kiroho yanatambuliwa na roho.

"Lakini Mwokozi hakwenda na hoja kwa hoja. Akiunyoosha mkono wake kwa nguvu, kwa heshima, aliubandika ukweli mahali pake kwa uhakika mkubwa, akasema, "Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu." — *The Desire of Ages*, p. 171.

**b. Mtu anaweza kuzaliwa mara ya pili lini na kwa jinsi gani? Yohana 1:12, 13.**

" 'Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee; ili mwanadamu apatanishwe na Mungu. Kupitia wema wa kristo anaweza kurejeshwa kwenye upatano na muumba wake. Moyo wake lazima ufanywe upya kwa neema ya kimungu; lazima awe na maisha kutoka juu. Mabadiliko haya ni kuzaliwa upya, bila hivyo, asema Yesu, 'hawezi kuuona ufalme wa Mungu."— *The Great Controversy,* p. 467.

"Kupitia [tendo] rahisi la kumwamini Mungu, Roho Mtakatifu amezaa maisha mapya moyoni mwako. Wewe ni kama mtoto aliyezaliwa katika familia ya Mungu, na Yeye anakupenda kama anavyompenda Mwanawe." — *Steps to Christ*, p. 52.

**a. Ni nini kinachoashiria utakaso na kufanywa upya unaokuja na kuzaliwa upya? Marko 16:16 (sehemu ya kwanza).**

---

---

"Nguvu ya Mungu ya kuongoa inaweza kubadilisha mielekeo iliyorithiwa na kusitawishwa; kwani dini ya Yesu inainua. 'Kuzaliwa mara ya pili' kunamaanisha kubadilishwa, kuzaliwa upya katika Kristo Yesu." — *The Adventist Home,* p. 206.

"Kristo amefanya ubatizo kuwa ishara ya kuingia katika ufalme wake wa kiroho. Amefanya hili kuwa sharti chanya ambalo wote wanapaswa kufuata wale wanaotaka kutambuliwa kuwa chini ya mamlaka ya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Kabla ya mwanadamu kupata makao katika kanisa, kabla ya kupita kizingiti cha ufalme wa kiroho wa Mungu, anapaswa kupokea mkazo wa jina la kimungu, 'Bwana, ni haki Yetu.' Yeremia 23:6.

"Ubatizo ni kuukana kabisa ulimwengu. Wale wanaobatizwa katika Jina lenye sehemu tatu la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, kwenye mlango wa kuingia kabisa wa maisha yao ya Kikristo wanatangaza hadharani kwamba wameacha utumishi wa Shetani na wamekuwa washiriki wa familia ya kifalme, watoto wa Mungu. Mfalme wa mbinguni. Wametii amri: "Tokeni miongoni mwao, na jitengeni... wala msiguse kitu kilicho najisi. Na kwao inatimia ahadi: "Mimi nitawakaribisha, Nami nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa Kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi." 2Wakorintho 6:17, 18." — *Testimonies for the Church,* vol. 6, p. 91.

**b. Ni nini kinachotangazwa kuhusu uovu wa asili yetu ya kibinadamu na mpango wa Mungu wa kutubadilisha? Yohana 3:6; Yeremia 17:9; Waefeso 5:26, 27.**

---

---

---

"Haiwezekani sisi, sisi wenyewe, kuepuka shimo la dhambi ambalo tumezama ndani yake. Mioyo yetu ni mibaya, na hatuwezi kuibadilisha. Elimu, utamaduni, utekelezaji wa nia, juhudi za kibinadamu, vyote vina nyanja zao sahihi, lakini hapa havina nguvu. Wanaweza kuzalisha usahihi wa nje wa tabia, lakini hawawezi kubadilisha moyo; hawawezi kutakasa chemchemi za uzima. Lazima kuwe na nguvu inayofanya kazi kutoka ndani, maisha mapya kutoka juu, kabla ya wanadamu kubadilishwa kutoka dhambi hadi utakatifu. Nguvu hiyo ni Kristo. Neema yake pekee ndiyo inayoweza kuhuisha nguvu zisizo na uhai za nafsi, na kuivuta kwa Mungu, kwenye utakatifu." — *Steps to Christ,* p.18.

## 5. MAISHA MAPYA NA MATENDO MAPYA 1/30 (Alhamis)

**a. Ni ujumbe gani ambao mitume walipaswa kuandika baadaye kuhusu badiliko la kuzingatia linalokuja na kuzaliwa upya? Wagalatia 2:20; 1Yohana 2:15 – 17.**

---

"Nguvu ya Mungu ya kuongoa inaweza kubadilisha mielekeo iliyorithiwa na kusitawishwa; kwani dini ya Yesu inainua. 'Kuzaliwa mara ya pili' kunamaanisha kubadilishwa, kuzaliwa upya katika Kristo Yesu." — *The Adventist Home,* p. 206.

"[Paulo] Alikuwa na hakika kwamba ikiwa akili za wanadamu zingeweza kuletwa ili kufahamu dhabihu ya ajabu iliyotolewa na Ukuu wa mbinguni, ubinafsi wote ungeondolewa mioyoni mwao. Anaelekeza akili kwanza kwenye nafasi ambayo Kristo alikuwa Nayo mbinguni, katika kifua cha Baba Yake; Anamdhihirisha baadaye kama anayeweka mbali utukufu Wake, kwa hiari Yake Mwenyewe chini ya hali zote za unyonge za asili ya mwanadamu, akichukua majukumu ya mtumwa, na kuwa mtiifu hadi kifo, na tena kifo ambacho ni cha aibu na maasi, cha maafa makubwa zaidi, chenye maumivu - kifo cha msalaba. Je, Wakristo wanaweza kutafakari onesho hili la ajabu la upendo wa Mungu kwa mwanadamu bila hisia za upendo na kutambua Ukweli kwamba sisi si mali yetu wenyewe? Bwana wa namna hiyo hatakiwi kutumikiwa kwa mielekeo yenye kinyongo, uchoyo na ubinafsi." — *Testimonies for the Church,* vol. 4, p. 458.

"Ningewaeleza kama Kristo alivyomwambia Nikodemo: "Lazima mzaliwe mara ya pili." Wale ambao Kristo anatawala ndani yao hawatahisi hamu ya kuiga maonesho ya ulimwengu. Wao kila mahali watabeba kiwango cha msalaba, daima watakuwa wamebeba ushuhuda wa hali ya juu na dhamira bora kuliko zile ambazo zimewameza walimwengu. Mavazi yetu, makao yetu, mazungumzo yetu, yanapaswa kushuhudia kujitoa kwetu kwa Mungu. Ni nguvu kubwa kiasi gani ambayo ingekuwa juu wale waliothibitisha kwamba wametoa vyote kwa ajili ya Kristo." — *Ibid.*, vol. 5, p. 189.

## 6. MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI 1/31 (Ijumaa)

**1. Kwa sababu ya matendo yake mema, Nikodemo alijionaje mwenyewe?**
**2. Nikodemo alitendaje mbele ya Kristo?**
**3. Je, ina maana gani "kuzaliwa mara ya pili"?**
**4. Je, kuzaliwa upya kunatokeaje?**
**5. Ni badiliko gani la mtazamo linalotokea baada ya kuzaliwa upya, na kwa nini?**

Sabato, Februari 8, 2025

**Somo la 6**

# Mguso wa Roho Mtakatifu

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa, ili kila mtu aaminiye, awe na uzima wa milele" (Yohana 3:14, 15).

**Inapendekezwa kusoma:** *Christ's Object Lessons,* pp. 95–102.

"Angalia, Ee mtazame Yesu na uishi!" — *Christian Education*, p. 76.

## 1. KUHUSIKA MASWALI — 2/2 (Sun)

**a. Ni swali gani la Nikodemo linaloonyesha kwamba moyo wake ulikuwa ukilainika? Yohana 3:9.**

---

---

---

"Yesu kwa hakika anamwambia Nikodemo: Si ubishi utakaosaidia kesi yako: si mabishano yatakayoleta nuru kwa nafsi. Lazima uwe na moyo mpya, au huwezi kutambua ufalme wa mbinguni. Sio ushahidi mkubwa zaidi ambao utakuleta katika nafasi sahihi, lakini nia mpya, chemchemi mpya za utendaji. Ni lazima kuzaliwa mara ya pili. Hadi badiliko hili lifanyike, kufanya mambo yote kuwa mapya, ushahidi wenye nguvu zaidi ambao ungeweza kuwasilishwa hautakuwa na maana. Uhitaji uko moyoni mwako; kila kitu lazima kibadilishwe, au huwezi kuuona ufalme wa Mungu.

"Hii ilikuwa kauli ya kumfedhehesha sana Nikodemo. Hakuwa hivyo wenye nia ya kiroho vya kutosha kutambua maana ya maneno ya Kristo. Lakini Mwokozi hakukutana na mabishano na mabishano. . . .

"Baadhi ya nuru za ukweli zilikuwa zikipenya akilini mwa mtawala huyo. Maneno ya Kristo yalimjaza hofu, na kupelekea kuuliza, 'Mambo haya yawezaje kuwa na bidii sana Yesu akajibu, Je! kwamba, badala ya kuhisi kuudhishwa na maneno ya wazi ya ukweli, na kujifurahisha kwa kejeli, anapaswa kuwa na maoni ya unyenyekevu zaidi juu yake mwenyewe, kwa sababu ya ujinga wake wa kiroho. Lakini maneno ya Kristo yalisemwa kwa heshima kubwa sana, na sura na sauti zote zilionyesha upendo wa dhati kwake, hata hakuchukizwa alipotambua nafasi yake ya kufedhehesha." — *Testimonies to Ministers,* pp. 368, 369.

**a. Mafarisayo walijivunia nini? Luka 18:9–12.**

“Wayahudi walikuwa wameitwa kwanza katika shamba la mizabibu la Bwana, na kwa sababu hiyo walikuwa na kiburi na kujiona kuwa waadilifu. Miaka yao mingi ya utumishi waliona kuwa inawawezesha kupokea thawabu kubwa kuliko wengine. Hakuna lililokuwa likiwakasirisha zaidi kuliko kudokeza kwamba watu wa Mataifa wangekubaliwa kuwa na mapendeleo sawa na wao wenyewe katika mambo ya Mungu.”—*Christ’s Object Lessons,* p. 400.

**b. Je, Yesu alionyeshaje kazi ya Roho Mtakatifu moyoni? Yohana 3:8.**

“Upepo husikika katika matawi ya miti, yakitikisa majani na maua na kuyafanya yatoe sauti; lakini hauonekani, na hakuna mtu anayejua unakotoka na unakokwenda. Hivyo ndivyo ilivyo kazi ya Roho Mtakatifu katika moyo. Haiwezi kuelezeka zaidi ya vile upepo uvumavyo. Mtu hawezi kueleza muda hasa au mahali, au kufuatilia mazingira yote ya kuongoka kwake; lakini hali hii haimfanyi kwamba awe hajaongoka. Kwa njia isiyoonekana kama ulivyo upepo, Kristo anafanya kazi na moyo wakati wote. ” — *The Desire of Ages*, p. 172.

**c. Mguso wa Uungu unawekwaje moyoni? Isaya 30:21; Yeremia 42:3; Mathayo 16:17.**

“Kidogo-kidogo, pengine bila mhusika kujua, mawazo ambayo yana tabia ya kuuvuta moyo kwa Yesu yanawekwa. Haya yanaweza kupatikana kwa kumtafakari Yesu, kwa kusoma Maandiko, au kwa njia ya kusikiliza neno moja kwa moja kwa mhubiri. Ghafla, kadiri Roho anavyokuja kwa ushawishi wa moja kwa moja, roho hujisalimisha kwa furaha kwa Yesu. Kwa wengi hali hii inaonekana kama uongofu wa ghafla; lakini ni matokeo ya kubembeleza kwa Roho wa Mungu kwa muda mrefu.”—Ibid.

“Ruhusu mioyo yenu kulainishwa na kutiishwa na Roho wa Mungu. Acha roho zilizofungwa kwenye barafu ziyeyuke chini ya utendaji kazi ya Roho Mtakatifu.” — *Letters and Manuscripts*, vol. 12, Letter 53, 1897.

## 3. USHAHIDI WA KUZALIWA UPYA — 2/4 (Jnne)

**a. Je, matendo ya ndani ya Roho Mtakatifu yanadhihirishwaje kwa nje? Wagalatia 5:22–25.**

---

---

"Wakati upepo kwa wenyewe hauonekani, unaleta matokeo ambayo yanaonekana na kuweza kuyahisi. Vivyo hivyo kazi ya Roho katika moyo itajifunua katika kila tendo la mtu ambaye amepokea nguvu yake iokoayo. Wakati Roho Mtakatifu anapoumiliki moyo, anabadilisha maisha. Mawazo ya dhambi yanawekwa mbali, matendo maovu yanaachwa; upendo, unyenyekevu, na amani vinachukua nafasi ya hasira, husuda, na magomvi. Furaha huchukua nafasi ya huzuni, na uso huakisi nuru ya mbinguni. Hakuna mtu anayeona mkono unaobeba mzigo, au kuona nuru inavyoshuka kutoka mbinguni juu. " — *The Desire of Ages*, p. 173.

**b. Ni wakati gani mtu anapokea baraka ya mabadiliko? Warumi 10:9,10; 1Yohana 1:9.**

---

---

"Hakuna mtu anayeona mkono unaobeba mzigo, au kuona nuru inavyoshuka kutoka mbinguni juu. Mbaraka unakuja pindi moyo unapojisalimisha kwa imani kwa Mungu. Hapo nguvu ile ambayo haiwezi kuonekana kwa jicho la mwanadamu huumba utu upya katika sura ya Mungu." — Ibid.

"Ikiwa una Roho Mtakatifu akiutengeneza na kuutengeneza moyo wako kila siku, basi utakuwa na utambuzi wa kiungu wa kutambua tabia ya ufalme wa Mungu. Nikodemo alipokea somo la Kristo na akawa muumini wa kweli." — *Testimonies to Ministers*, ukurasa wa 369, 370.

**c. Kristo anaonyeshaje mchakato huu? Mathayo 13:33.**

---

---

"Chachu iliyofichwa ndani ya unga hufanya kazi bila kuonekana ili kuleta donge zima chini ya uchachu wake; hivyo chachu ya ukweli hutenda kazi kwa siri, kimya kimya, kwa uthabiti, kuibadilisha nafsi. Mielekeo ya asili ni laini na inatiishwa. Mawazo mapya, hisia mpya, nia mpya, hupandikizwa. Kiwango kipya cha tabia kinawekwa—maisha ya Kristo. Akili inabadilishwa; vitivo vinaamshwa kuchukua hatua katika mistari mipya. Mwanadamu hajajaliwa uwezo mpya, lakini uwezo alionao umetakaswa. Dhamiri inaamshwa. Tumejaliwa kuwa na tabia zinazotuwezesha kumtumikia Mungu." — *Christ's Object Lessons,* pp. 98, 99.

## 4. MFANO UNAOFAHAMIKA 2/5 (Jtan)

**a. Je, Yesu alionyeshaje kusulubishwa kwake ambako kungelitokea karibuni? Yohana 3:14,15.**

"[Yohana 3:14, 15 imenukuliwa] Huu ulikuwa uwanja uliokuwa unafahamika kwa Nikodemo. Ishara ya nyoka aliyeinuliwa iliweka kwake uwazi wa kazi ya Yesu. Wakati watu wa Israeli walipokuwa wanakufa kwa kuumwa na nyoka wa moto, Mungu alimwagiza Musa kufanya nyoka wa shaba, na kumtundika juu katikati ya kusanyiko. Halafu tangazo lilitolewa katika mahema yote kwamba wote ambao wangemwangalia yule nyoka wangeishi. Watu walijua vema kwamba yule nyoka hakuwa na uwezo ndani yake mwenyewe wa kuwasaidia. Alikuwa ishara ya Kristo. Kama vile sanamu ile ya nyoka iliyofanywa katika mfano wa nyoka aharibuye ilivyoinuliwa juu kwa ajili ya uponyaji wao, ndivyo ambavyo Yeye aliyefanywa "katika mfano wa mwili ulio wa dhambi" angekuwa Mkombozi. Warumi 8:3. Wengi miongoni mwa Waisraeli walichukulia kwamba huduma za kafara zilikuwa na uwezo wa kuwaweka huru kutoka katika dhambi. Mungu alitaka kuwafundisha kwamba hazikuwa na thamani tena zaidi ya vile alivyokuwa nyoka wa shaba. Lengo lilikuwa ni kuongoza mawazo yao kwenda kwa Mwokozi. Iwe ni kwa kuponya majeraha yao au kusamehewa dhambi zao, wasingejifanyia lolote bali kuonyesha imani yao katika Zawadi ya Mungu. Walipaswa waiangalie ili waishi." — *The Desire of Ages*, pp. 174, 175.

**b. Licha ya neema hio, kwa nini wengine walikufa? 1Wakorintho 10:9; Waebrania 3:12.**

"Wengi wa Waisraeli hawakuona msaada wowote katika dawa ambayo Mbingu ilikuwa imeweka. Wafu na wanaokufa walikuwa wamewazunguka pande zote, na walijua kwamba, bila msaada wa kimungu, hatima yao wenyewe ilikuwa hakika; lakini waliendelea kuomboleza majeraha yao, maumivu yao, kifo chao cha hakika, hadi nguvu zao zilipokwisha, na macho yao yakang'aa, wakati wangeweza kupata uponyaji wa papo hapo." — *Patriarchs and Prophets*, p. 432.

**c. Ikiwa tunataka kuokolewa, tunapaswa kuangalia wapi? Waebrania 6:19, 20.**

"Madhara mabaya ya dhambi yanaweza kuondolewa tu kwa utoaji ambao Mungu amefanya. Waisraeli waliokoa maisha yao kwa kumtazama yule nyoka aliyeinuliwa. Muonekano huo ulimaanisha imani. Waliishi kwa sababu waliamini neno la Mungu, na kutumainia njia zilizotolewa kwa ajili ya kupona kwao. Kwa hiyo mwenye dhambi anaweza kumwangalia Kristo, na kuishi. Anapokea msamaha kupitia imani katika dhabihu ya upatanisho. Kristo ana nguvu na wema ndani yake kuwaponya wenye dhambi wanaotubu." — *Ibid.*, p. 431.

## 5. KUKAZA MACHO YETU — 2/6 (Alhamis)

a. Ni somo gani ambalo baadaye lilieleweka na Nikodemo tunalohitaji kulichukua—na kukumbuka daima? Waefeso 2:8; Luka 13:2,21.

---

---

"Mara nyingi swali hutokea, Kwa nini, basi, kuna watu wengi sana, wanaodai kuamini neno la Mungu, ambao ndani yao hauonekani matengenezo katika maneno, katika roho, na katika tabia? Kwa nini kuna wengi sana ambao hawawezi kustahimili upinzani kwa madhumuni na mipango yao, wanaodhihirisha hasira isiyo takatifu, na ambao maneno yao ni makali, ya kupita kiasi, na ya shauku? Kunaonekana katika maisha yao mapenzi yale yale ya nafsi, ubinafsi uleule, hasira sawa na usemi wa haraka, unaoonekana katika maisha ya walimwengu. Kuna majivuno yale yale nyeti, yale yale kujitoa kwa mwelekeo wa asili, upotovu uleule wa tabia, kana kwamba ukweli haujulikani kwao kabisa. Sababu ni kwamba hawajaongoka. Hawajaficha chachu ya ukweli moyoni. Haijapata nafasi ya kufanya kazi yake. Mielekeo yao ya asili na iliyokuzwa kwa uovu haijatiishwa kwa nguvu zake za kubadilisha. Maisha yao yanaonyesha kutokuwepo kwa neema ya Kristo, kutokuamini katika uwezo wake wa kubadilisha tabia.

" 'Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo.' Warumi 10:17. Maandiko ni wakala mkuu katika mabadiliko ya tabia. Kristo aliomba, 'Uwatakase kwa ile kweli ; Neno lako ndiyo kweli.' Yoh. 17:17 . Kama likisomwa na kutiiwa, neno la Mungu linafanya kazi moyoni, likishinda kila sifa isiyo takatifu. Roho Mtakatifu huja kuhukumu dhambi, na imani inayochipuka ndani ya moyo hufanya kazi kwa upendo kwa Kristo, akitufananisha sisi katika mwili, nafsi na roho na sura yake mwenyewe. Kisha Mungu anaweza kututumia kufanya mapenzi yake. Nguvu tuliyopewa hufanya kazi kutoka ndani na nje, ikituongoza kuwasilisha kwa wengine ukweli ambao umewasilishwa kwetu." — *Christ's Object Lessons,* pp. 99, 100.

## 6. MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI — 2/7 (Ijumaa)

1. Ni nini ilikuwa sifa kuu ya Mafarisayo katika siku za Kristo?
2. Eleza jinsi tunavyofanywa upya katika kufanana na Kristo.
3. Je, mabadiliko ya moyo yanadhihirikaje?
4. Eleza ishara ya nyoka aliyeinuliwa.
5. Je, mfano wa chachu unadhihirishaje kukua kwa neema ya Mungu?

Sabato, Februari 15, 2025

**Somo la 7**

# Yesu na Yohana Mbatizaji

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Yeye hana budi kuzidi, bali mimi kupungua" (Yohana 3:30).

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 5, pp. 721–729.

"Yohana Mbatizaji alitangazwa na Mwokozi wetu ya kuwa mkuu wa manabii. Lakini kuna utofauti mkubwa kiasi gani wa usemi kati ya huyu mtu wa Mungu na wa wale wengi wanaodai kuwa wahudumu wa msalaba. Alipoulizwa ikiwa yeye ndiye Kristo, Yohana anajitangaza mwenyewe kuwa hastahili hata kufungua viatu vya Bwana Wake."—*Testimonies for the Church*, vol. 5, p. 224.

## 1. TATIZO MIONGONI MWA WANAFUNZI — 2/9 (Jpil)

**a. Ni swali gani lilizuka kati ya wanafunzi wa Yohana na Wayahudi? Yohana 3:25.**

---

"Lakini wanafunzi wa Yohana walipatwa na wivu kwa sababu umaarufu wa Yesu ulikuwa unaongezeka sana. Walijiweka tayari kuikosoa kazi yake, nahaukupita muda mrefu kabla ya wao kupata fursa hiyo. Swali liliibuka kati yao na Wayahudi likiuliza ikiwa ubatizo ulilenga kutakasa moyo dhidi ya dhambi; wao wakashikilia msimamo kwamba ubatizo wa Yesu ulitofautiana na ule wa Yohana. Baada ya muda mfupi kulikuwa na mabishano kati yao na wanafunzi wa Yesu kuhusu maneno yanayofaa kutumiwa wakati wa kubatiza, na mwishowe wakahoji uhalali wa huo ubatizo mwingine. " — *The Desire of Ages,* p. 178.

**b. Wanafunzi wa Yohana walionyeshaje wivu wao juu ya kazi ya Kristo — na ni jibu gani zuri alilotoa? Yohana 3:26, 27.**

---

"Kwa asili Yohana alikuwa na mapungufu na udhaifu wa kawaida kwa mwanadamu, lakini mguso wa upendo wa kimbingu ulikuwa umembadilisha. Alikuwa amekaa katika mazingira ambayo hayakuchafuliwa na ubinafsi na tamaa ya kutaka makuu, na zaidi sana tatizo la wivu. Hakuonyesha huruma kwa kutoridhishwa kwa wanafunzi wake, bali alionyesha jinsi ambavyo alielewa uhusiano wake na Masihi, na jinsi alivyomkaribisha kwa furaha Yeye ambaye alikuwa amemtayarishia njia." – *Ibid.,* p.179.

## 2. UTUME WA YOHANA 2/10 (Jtat)

**a. Yohana alionyeshaje kwamba alielewa utume wake? Yohana 3:28, 29.**

---

“Kwa asili Yohana alikuwa na mapungufu na udhaifu wa kawaida kwa mwanadamu, lakini mguso wa upendo wa kimbingu ulikuwa umembadilisha. Alikuwa amekaa katika mazingira ambayo hayakuchafuliwa na ubinafsi na tamaa ya kutaka makuu, na zaidi sana tatizo la wivu. Hakuonyesha huruma kwa kutoridhishwa kwa wanafunzi wake, bali alionyesha jinsi ambavyo alielewa uhusiano wake na Masihi, na jinsi alivyomkaribisha kwa furaha Yeye ambaye alikuwa amemtayarishia njia. ” — *The Desire of Ages,* p. 179.

**b. Elezea kazi ya Yohana — na yetu. Yohana 1:23, 29.**

---

“Akimwangalia Mkombozi kwa imani, Yohana alikuwa amefika juu katika kilele cha kujinyima. Hakutafuta kuwavuta watu kwake mwenyewe, bali kuinua mawazo yao juu na juu zaidi, mpaka yatulie kwa Mwanakondoo wa Mungu. Yeye alikuwa amekuwa sauti tu, kilio cha nyikani. Sasa kwa furaha alikubali kufichika na kutoonekana yeye, ili ya kwamba macho ya wote yapate kugeuzwa kuielekea Nuru ya uzima.

“Wale ambao ni wakweli kwa wito wao kama wajumbe kwa ajili ya Mungu hawatatafuta heshima zao wenyewe. Kujipenda wenyewe kutakuwa kumemezwa katika kumpenda Yesu. Kwao hakuna kushindana ambako kutaharibu njia ya thamani ya injili. Watagundua kwamba kazi yao ni kuwatangazia watu, kama alivyofanya Yohana Mbatizaji, kwamba ”Tazama Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.” 1Yohana 1:29. Watamwinua Yesu, na ndani yake uanadamu utainuliwa juu. “Maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye jina lake ni Mtakatifu; asema hivi; Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu; tena pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu.” Isaya 57:15. — *Ibid*., pp. 179, 180.

“Usitafute radhi na manufaa yako mwenyewe, bali tafuta kujua na kufanya mapenzi ya Mungu. Hebu kila mmoja aulize, Je, siwezi kuelekeza nafsi fulani kwa Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu? Je, siwezi kumfariji mtu aliyekata tamaa? Je, siwezi kuwa njia ya kuokoa nafsi fulani katika ufalme wa Mungu? Tunataka mienendo ya kina ya Roho wa Mungu mioyoni mwetu, ili tuweze sio tu kujiwekea mavazi meupe, bali tuweze kuwashawishi wengine ili majina yao yaingizwe katika kitabu cha uzima, yasifutike kamwe.” — *Historical Sketches*, p. 140.

## 3. KIPAWA CHA ROHO 2/11 (Jnne)

**a. Watu wengi waliitikiaje ujumbe wa Kristo? Yohana 3:32.**

“Wanafunzi wa Yohana walikuwa wamesema kwamba watu wote walikuwa wanakwenda kwa Kristo; lakini kwa muono wa wazi zaidi, Yohana alisema, „Hakuna anayeukubali ushuhuda wake;” kwa hiyo wachache ndio walikuwa tayari kumkubali kama Mwokozi wa kutoa watu dhambini. Lakini „yeye aliyeukubali ushuhuda wake ametia muhuri ya kwamba Mungu ni kweli.” Yohana 3:33. — *The Desire of Ages*, p. 181.

**b. Ni juu ya nani hupewa kipawa cha Roho Mtakatifu? Yohana 3:34.**

“Tunaweza kupokea nuru ya mbinguni ikiwa tu tuna utashi wa kubaki watupu tukiwa tumeondoa ubinafsi. Hatuwezi kutambua tabia ya Mungu, au kumpokea Yesu kwa imani, tusipokubali hali ya kila wazo kushikiliwa mateka kwa kuletwa katika utii wa Kristo. Kwa wote wafanyao haya Roho Mtakatifu hutolewa bila kipimo. Katika Kristo „unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. Na ninyi mmetimilika katika yeye.” Wakolosai 2:9, 10. — Ibid.

**c. Ni kwa Jinsi gani huwa ni ufunguo wa kupokea kipimo kikubwa zaidi cha Roho Mtakatifu kama ilivyofunuliwa zaidi katika Maandiko? Yohana 14:15–17; Matendo 5:32.**

“Hatupaswi kusema tu, “Naamini,” bali kutenda Ukweli. Ni kwa kupatana na mapenzi ya Mungu katika maneno yetu, mwenendo wetu, tabia zetu, ndipo tunapothibitisha uhusiano wetu Naye. Wakati wowote mtu anapoacha dhambi, ambayo ni uvunjaji wa sheria, maisha yake yataletwa katika kupatana na sheria, katika utii mkamilifu. Hii ni kazi ya Roho Mtakatifu. Nuru ya Neno iliyosomwa kwa uangalifu, sauti ya dhamiri, jitihada za Roho, huzalisha ndani ya moyo upendo wa Kweli kwa Kristo, ambaye alijitoa mwenyewe dhabihu nzima ili kumkomboa mtu mzima, mwili, nafsi na roho. Na upendo unadhihirika katika utiifu. Mstari wa kuweka mipaka utakuwa wazi na tofauti kati ya wale wanaompenda Mungu na kuzishika amri Zake, na wale wasiompenda na kupuuza maagizo Yake. ” — *Testimonies for the Church*, vol. 6, p. 92.

## 4. THAMANI YA UBATIZO

2/12 (Jtano)

**a. Kwa nini ni muhimu kuelewa hatua tunayochukua kwa ajili ya Kristo tunapoamua kubatizwa? Yohana 3:36.**

---

"Mbali na Kristo, ubatizo, kama ilivyo huduma nyingine yoyote ya kidini, ni desturi isiyo na thamani. " — *The Desire of Ages,* p. 181.

"Hakuna sababu ya malumbano kwamba labda ubatizo wa Kristo au wa Yohana ulitakasa kutokana na dhambi. Ni neema ya Mungu inayotoa uzima kwa roho. " — Ibid.

"Ni kwa njia ya kristo tu kutoweza kufa kunaweza kupatikana. Yesu alisema hivi: 'Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele, asiyemwamini Mwana hataona uzima.'Yohana 3:36. Kila mtu anaweza kumiliki baraka hii isiyokadirika ikiwa atatii masharti. 'Wale ambao kwa saburi katika kutenda mema wakitafuta utukufu na heshima na kutokuharibika,' watapewa 'uzima wa milele.' Warumi 2:7." — *The Great Controversy*, p. 533.

"Ubatizo ni kuukana kabisa ulimwengu. Wale wanaobatizwa katika Jina lenye sehemu tatu la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, kwenye mlango wa kuingia kabisa wa maisha yao ya Kikristo wanatangaza hadharani kwamba wameacha utumishi wa Shetani na wamekuwa washiriki wa familia ya kifalme, watoto wa Mungu. Mfalme wa mbinguni." — *Testimonies for the Church*, vol. 6, p. 91.

**b. Elezea maneno ya kustaajabisha ya Yohana Mbatizaji ambayo yalifunua kina halisi cha maisha ya kujitoa kinachoonyeshwa na ubatizo? Luka 3:7,8.**

---

---

---

"Yohana aliweka shoka katika shina la mti. Alikemea dhambi, bila kuogopa matokeo yake, na kutayarisha njia kwa ajili ya Mwanakondoo wa Mungu.

"Herode alivutiwa kwa kadri alivyosikia ushuhuda wenye nguvu, uliotolewa na Yohana, na kwa shauku kuu aliuliza afanye nini ili awe mwanafunzi wa wake. Yohana alitambua ukweli kwamba Herode alikuwa karibu amwoe mke wa ndugu yake wakati mumewe akiwa bado hai, na kwa uaminifu alimwambia si haki! " — *Early Writings,* p. 154.

"Yohana Mbatizaji alikabili dhambi kwa karipio la wazi kwa watu wa wadhifa wa chini na watu wa nyazifa za juu. Alitangaza ukweli kwa wafalme na wakuu, ikiwa wangeisikia au kuikataa. Alitaja nafsi moja kwa moja." — *Selected Messages*, bk. 2, p. 149.

## 5. MBINU YA HEKIMA 2/13 (Alhamis)

**a. Alipotambua kwamba Mafarisayo walikuwa wakijaribu kuleta mgogoro kati ya Yohana na Yeye Mwenyewe, Yesu alifanya nini? Yohana 4:1–3.**

---

"Yesu alijua kwamba wasingebakiza hata jitihada moja katika kutengeneza mgawanyiko kati ya wanafunzi wake na wale wa Yohana. Alijua kwamba dhoruba ilikuwa inakusanyika ili kumkumba mmoja wa manabii wakuu mno waliopata kutolewa kwa ulimwengu. Akitaka kuepusha matukio yote ambayo yangesababisha mfarakano au mgawanyiko, Yesu aliachana na kazi yake, na akaondoka kwenda Galilaya. Hata sisi pia tunatakiwa kukwepa yale yote yanayoweza kuleta upinzani na uelewa usio sahihi, huku tukidumu kuwa waaminifu kwa ukweli. Maana kila yanapoibuka haya, matokeo yake ni upotevu wa roho. Wakati wowote mazingira yanayotishia kusababisha mgawanyiko yanapotokea, tunapaswa kufuata mfano wa Yesu na wa Yohana Mbatizaji."—*The Desire of Ages,* p. 181.

**b. Je, tunapaswa kujifunza nini kutokana na mtazamo wa Yohana wa kutatua mgogoro? Yohana 3:30.**

---

"Kama walivyokuwa wanafunzi wa Yohana, wengi hufikiri kwamba mafanikio ya kazi yanategemea mtenda-kazi yule wa kwanza. Mawazo yanakazwa kwa mwanadamu badala ya Mungu, wivu unakuja, na kazi ya Mungu inapata vikwazo. Yule anayetukuzwa hivyo kupita kiasi anajaribiwa kutegemea uwezo wake mwenyewe. Hatambui utegemezi wake kwa Mungu. Watu wanafundishwa kumwangalia mtu kama kiongozi, na kwa njia hiyo wanaanguka katika makosa, nao wanaongozwa kwenda mbali na Mungu.

"Kazi ya Mungu isipewe sura wala alama ya mwanadamu. Katika vipindi tofauti Mungu ataleta mawakala tofauti, ambao kupitia kwao kusudi lake linaweza kukamilishwa kwa mafanikio. Wana furaha wale ambao wanakubali nafsi zao zishushwe, wakisema pamoja na Yohana Mbatizaji kwamba, "Yeye hana budi kuzidi, bali mimi kupungua." — *Ibid.*, p. 182.

## 6. MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI 2/14 (Ijumaa)

1. Kwa nini wanafunzi wa Yohana waliionea wivu kazi ya Kristo?
2. Yohana alitangaza nini kwa wanafunzi wake?
3. Kipawa cha Roho Mtakatifu kinatolewa kwa kusudi gani?
4. Ubatizo unatimizaje lengo lake la kweli?
5. Yesu na Yohana walifanya nini walipotambua hatari ya mgogoro kati ya wanafunzi wao?

Sabato, Februari 22, 2025

**Somo la 8**

# Yesu na Mwanamke Msamaria

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Walakini ye yote atakayekunywa maji nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele" (Yohana 4:14).

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 4, pp. 384–387.

"Yeye anayetafuta kupoza kiu yake katika visima vya ulimwengu huu atakunywa na kuona kiu tena. Kila mahali wanadamu hawatosheki. Wanatafuta kitu cha kuleta mahitaji ya moyo. Ni Mmoja tu anayeweza kukidhi mahitaji hayo. Hitaji la ulimwengu, Tumaini la mataifa yote, ni Kristo. "—*The Desire of Ages,* p. 187.

## 1. YESU AKIWA SIKARI 2/16 (Jpil)

**a. Katika safari yake ya kwenda Galilaya, Yesu na wanafunzi wake walisimama wapi? Yohana 4:6.**

---

"Yesu alipokuwa amekaa kando ya kisima, alikuwa na nja na kiu. Safari ya tangu asubuhi ilikuwa ndefu, na sasa alikuwa anapigwa na jua la mchana-kati. Kiu yake iliongezwa zaidi na mawazo ya uwepo wa maji baridi ya kuburudisha pale karibu, lakini akiwa hawezi kuyafikia; maana alikuwa hana kamba wala chombo cha kuchotea, na kisima kilikuwa na kina kirefu. Alikuwa na hali ya ubindamu, na alisubiri mtu aje achote maji. " — *The Desire of Ages,* p. 183.

**b. Ni nani aliyekuja kwenye kisima, na Yesu alimwomba nini—na tunapaswa kujifunza nini kutokana na hilo? Yohana 4:7.**

---

"Chuki iliyokuwepo kati ya Wayahudi na Wasamaria ilimzuia yule mwanamke kumfanyia ukarimu ule Yesu; lakini Mwokozi alikuwa anatafuta kupata ufunguo wa kuingilia katika moyo huu, na kwa mbinu yenye upendo wa kimbingu, aliomba fadhila, si kutoa fadhila. Ile fadhila ya ukarimu ingeweza kukataliwa; lakini tumaini huamsha tumaini. Mfalme wa mbinguni aliijia nafsi hii ya mwanamke iliyotengwa mbali, akiomba huduma mikononi mwake. Yeye aliyefanya bahari, anayetawala vilindi vya maji, aliyefungua chemchemi za maji na mifereji ya nchi, alijipumzisha panapo kisima cha Yakobo kwa uchovu, na alikuwa mtegemezi wa ukarimu wa mgeni kwa zawadi ya maji ya kunywa. " – *Ibid.*, p.184.

## 2. AINA TOFAUTI YA MAJI — 2/17 (Jtatu)

**a. Je, Yesu alielekeza jinsi gani usikivu wa mwanamke kwenye karama ya wokovu? Yohana 4:10.**

"Maji ambayo Kristo aliyataja yalikuwa ni ufunuo wa neema yake katika neno lake; Roho wake, mafundisho yake, ni kama chemchemi ya kuridhisha kwa kila nafsi. Kila chanzo kingine watakachokimbilia hakitoshi. Lakini neno la ukweli ni kama vijito baridi, vinavyowakilishwa kama maji ya Lebanoni, ambayo yanaridhisha kila wakati. Katika Kristo ni utimilifu wa furaha milele." — *Testimonies to Ministers,* p. 390.

**b. Je, mwanamke aliitikiaje pendekezo la Kristo? Yohana 4:11,12.**

"Ufahamu wa mwanamke haukuelewa maana ya Kristo; alidhani kwamba alikuwa akizungumza juu ya kisima kilichokuwa mbele yao."— *The Spirit of Prophecy,* vol. 2, pp. 140, 141.

**c. Je, Yesu alitofautishaje kati ya aina moja ya maji na nyingine—na ni jinsi gani ujumbe huu utatubariki sisi pia? Yohana 4:13, 14; Ufunuo 22:17.**

"Tunapaswa kuthamini upendo na shukrani, tunapaswa kumwangalia Yesu na kubadilishwa kuwa mfano Wake. Matokeo ya hili yataongezeka kujiamini, matumaini, subira, na ujasiri. Tutakunywa maji ya uzima ambayo Kristo alizungumza na mwanamke wa Samaria. Alisema: 'Kama ungalijua karama ya Mungu, na ni nani akuambiaye, Nipe maji ninywe; ungemwomba, naye angalikupa maji yaliyo hai yeyote atakayekunywa katika maji nitakayompa.........hawataona kiu kamwe; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele.' Maji haya yanawakilisha uzima wa Kristo, na kila nafsi lazima iwe nayo kwa kuingia katika uhusiano wa kuishi pamoja na Mungu. Kisha kubarikiwa, unyenyekevu, ujasiri wa shukrani utakuwa kanuni ya kudumu katika nafsi. Hofu ya kutokuamini itafagiliwa mbali kabla ya imani hai. Tutafakari tabia yake yeye aliyetupenda kwanza." — *Testimonies to Ministers,* p. 226.

## 3. MAJI HAI 2/18 (Jnne)

**a. Mwanamke Msamaria alionyeshaje kwamba bado hakuelewa maneno ya Kristo? Yohana 4:15.**

“Neema ya kimbingu ambayo inaweza kutolewa na Yeye tu, ni maji ya uzima, yasafishayo, yaburudishayo, na kuutia moyo nguvu.

“Maana aliyotoa Yesu si kwamba maji ya kunywa mara moja tu yangemtosha yeye aliyeyapokea. Yeye anayeonja upendo wa Kristo ataendelea kutamani zaidi; lakini hatafuti kitu kingine. Havutiwi na utajiri, ukuu, wala anasa za dunia. Kilio cha moyo wake wakati wote ni kusema, Zaidi kutoka kwako Bwana. Na Yeye anayeufunulia moyo yaliyo mahitaji ya moyo huo yuko tayari akisubiri ili kutosheleza njaa na kiu. Kila rasilimali-mtu na utegemezi

vitaanguka. Matanki ya maji yatabaki matupu, madimbwi yanakauka; lakini Mkombozi wetu ni kisima kisichoishiwa. Tunaweza kunywa, na kunywa, na kudumu kupata burudiko. Yeye ambaye anakuwa na Kristo ndani yake ana chemchemi ya baraka ndani yake mwenyewe, - “chemchemi ya maji yakibubujikia uzima wa milele.” Kutoka katika chanzo hiki anaweza kuchota nguvu na neema inayotosheleza mahitaji yake yote. ” — *The Desire of Ages,* p. 187.

**b. Kama vile mwanamke Msamaria na wasafiri wa jangwani katika Kutoka, ni kwa jinsi gani mara nyingi tunashindwa kutambua neema ya ajabu inayobubujika kutoka kwa Kristo? Zaburi 78:15,16,19,20 (sehemu ya kwanza); 114:7,8.**

“Musa aliupiga mwamba, lakini ni Mwana wa Mungu ambaye, akiwa amefunikwa kwenye nguzo ya wingu, alisimama kando ya Musa, na kusababisha maji ya kutoa uhai yatiririke. Si Musa tu, na wazee, bali na mkutano wote waliosimama mbali, wakauona utukufu wa Bwana; lakini kama lile wingu lingeondolewa, wangeliuawa kwa mwangaza wa kutisha wa yule aliyekaa humo.” — *Patriarchs and Prophets*, p. 298.

“Uwepo wa neema ya Kristo katika neno Lake daima ni kuzungumza na nafsi, ukimwakilisha Yeye kama kisima cha maji ya uzima ili kuiburudisha nafsi yenye kiu. Ni fursa yetu kuwa na Mwokozi aliye hai, anayedumu. Yeye ndiye chanzo cha nguvu za kiroho zilizopandikizwa ndani yetu, na mvuto Wake utatiririka kwa maneno na matendo, ukiwaburudisha wote ndani ya nyanja ya ushawishi wetu, ukizaa ndani yao matamanio ya nguvu na usafi, utakatifu na amani, na kwa ajili hiyo furaha ambayo haileti huzuni nayo. Haya ni matokeo ya Mwokozi anayekaa ndani yake.” — *Testimonies to Ministers*, p. 390.

## 4. YESU ANAANZA KUFUNUA UTAMBULISHO WAKE 2/19 (Jtan)

**a. Ni somo gani jipya ambalo Yesu alianzisha katika mazungumzo yake na mwanamke Msamaria—na mwanamke huyo aliitikiaje? Yohana 4:16, 17 (sehemu ya kwanza).**

"Sasa Yesu aligeuza maongezi. Kabla nafsi hii haijapokea zawadi aliyotaka kuipatia, lazima ifanywe kutambua dhambi yake na kumtambua Mwokozi wake. "Yesu akamwambia, Nenda kamwite mumeo, uje naye hapa." Mwanamke akajibu, "Sina mume." Hapo alitaka azuie maswali yote ambayo yangeelekezwa katika jambo hilo. " — *The Desire of Ages,* p. 187.

**b. Je, Yesu aliongezeaje jibu lake—na hii inatukumbusha nini kuhusu yote ambayo Yeye anajua kuhusu kila mmoja wetu? Yohana 4:17 (sehemu ya mwisho), 18; Zaburi 139:7, 8, 11, 12.**

"Ukuu wa Mungu kwetu sisi haueleweki. 'Kiti chake kiko mbinguni' ( Zaburi 11:4 ); lakini kwa Roho wake yuko kila mahali. Ana ujuzi wa ndani, na maslahi binafsi, katika kazi zote za mkono Wake." — *Education*, p. 132.

"Malaika wa mbinguni huchunguza kazi ambayo imewekwa mikononi mwetu; na pale ambapo kumekuwa na mgeuko kutoka kwa kanuni za ukweli, 'kutaka' kumeandikwa katika kumbukumbu." — *Child Guidance,* p. 155.

"Sheria ya Mungu hufikia hisia na nia, pamoja na matendo ya nje. Inafunua siri za moyo, inamulika nuru juu ya vitu kabla ya kuzikwa gizani. Mungu anajua kila wazo, kila kusudi, kila mpango, kila nia. Vitabu vya mbinguni vinaandika dhambi ambazo zingetendwa kama kungekuwa na nafasi. Mungu ataleta kila kazi hukumuni, pamoja na kila jambo la siri. Kwa sheria yake anapima tabia ya kila mtu. Msanii anapohamisha kwenye turubai vipengele vya uso, ndivyo vipengele vya kila mhusika huhamishiwa kwenye vitabu vya mbinguni. Mungu ana picha kamili ya tabia ya kila mtu, na picha hii Anailinganisha na sheria yake. Anamfunulia mwanadamu kasoro zinazoharibu maisha yake, na anamwita kutubu na kuacha dhambi." — *The SDA Bible commentary [E. G. White Comments],* vol. 5, p. 1085.

## 5. YESU ANAJIFUNUA KUWA NI MWOKOZI 2/20 (Alhamis)

**a. Mwanamke kisimani hatimaye alitambua nini kuhusu Yesu? Yohana 4:19. Je, utambuzi huu ulitosha?**

---

---

"Yule msikilizaji wake alitetemeka. Mkono wa siri ulikuwa unafunua kurasa za historia ya maisha yake, ukionyesha kile ambacho yule mwanamke alitamani kifichwe milele. Ni nani huyu ambaye aliweza kusoma siri za maisha yake? Mawazo ya umilele yalimjia yule mwanamke, ya kuhusu Hukumu ijayo, wakati ambapo yote yanayofichwa yatawekwa wazi. Katika hali hiyo, dhamiri iliamshwa.

"Hakuweza kukana kitu; lakini alijaribu kukwepa kutaja-taja habari hiyo isiyopendeza. Kwa heshima kubwa, alisema, "Bwana, naona ya kuwa u nabii!" halafu, akitaraji kunyamazisha hali ya kusadikishwa, aligeukia katika mambo ya kidini yanayotofautiana. Ikiwa huyu alikuwa nabii, kwa kweli angempa mafundisho kuhusu mambo haya ambayo yalikuwa yameleta mashaka. " — *The Desire of Ages,* pp. 187, 188.

**b. Mwanamke alipodhihirisha tumaini la kuja kwa Masihi, Yesu alimwambia nini? Yohana 4:25,26.**

---

---

"Mwaliko wa injili usifanywe kuwa finyu, na kuwasilishwa kwa wachache tu waliochaguliwa, ambao, tunadhani kwamba watatufaidi ikiwa wataipokea injili hiyo. Ujumbe utolewe kwa wote. Mahali popote ambapo mioyo iko wazi kupokea ukweli, Kristo yu tayari kuwafundisha. Anamfunua Baba kwao, na kuwafunulia ibada inayokubalika kwake Yeye asomaye moyo. Kwa hilo hatumii mafundisho kwa mifano. Kama ilivyokuwa kwa mwanamke pale kisimani, nao pia atawaambia, "Mimi ninayesema nawe ndiye." — *The Desire of Ages*, p. 194.

## 6. MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI 2/21 (Ijumaa)

1. Kwa nini Yesu hakufanya muujiza kwa niaba Yake mwenyewe?
2. Yesu alitumia nyenzo gani kumwongoza mwanamke Msamaria kwenye injili?
3. Mwalimu alisema nini kuhusu maji ya uzima?
4. Kwa nini Kristo alitaja maisha ya kibinafsi ya mwanamke Msamaria?
5. Taja ahadi inayohusishwa na ujio wa Masihi

# Sadaka za Sabato ya Kwanza

## Sabato, Machi 1, 2025

## “Watoto wa Tabia”

## Kituo cha Elimu nchini Romania




“Elimu ya mapema ya ujana kwa ujumla huunda tabia kwa maisha yote.” — *Testimonies for the Church*, vol. 3, p. 135.

“Msukumo unasimulia tukio la kutia moyo wakati “mikutano ya watoto, au shule ya chekechea ya Biblia, imefanya kazi nzuri. Masomo yanayotolewa yanarudiwa na watoto majumbani mwao, na akina mama wanaonyesha kupendezwa kwao kwa kuwatayarisha watoto vizuri kwa ajili ya shule. Wengi ni watoto wa wazazi sio wa imani yetu.”— *Evangelism,* p. 583.

“Kituo cha Elimu cha „Watoto wa Tabia” kilianzishwa mnamo 2019 huko Fagaras, mji wa mlima huko Romania. Watoto kati ya umri wa miaka 2 na 5 wanaendelea vizuri hapa. Mbali na shughuli maalum za umri, wao hujifunza hadithi za Biblia, kusali, kuimba na kumfanya Mungu kuwa rafiki yao. Wakiwa wachanga, wanaelewa kwamba Mungu ndiye anayetawala na wanajifunza kumwomba msaada kwa matatizo yao. Tabia zao hujengwa siku baada ya siku. Kwa neema ya Mungu tunaweza kuona mabadiliko ya ajabu katika maisha ya watoto hawa wadogo. Kwa siku zijazo, tungependa kuelimisha wale ambao hali yao ya nyenzo hairuhusu.

Mwaka wa kwanza tulianza na watoto 12; katika mwaka wa nne tulikuwa na watoto 32, 31 kati yao kutoka nje ya kanisa. Kwa sasa, shughuli hiyo inafanyika katika vyumba 4 vilivyotolewa katika Union ya Romania makao makuu, lakini haya yanaonekana kuwa na msongamano mkubwa kwani maombi ya uandikishaji ni zaidi ya uwezo wetu. Kwa hili, tunaelewa kwamba Mungu anataka tuendeleze na kuendeleza shughuli hii ya ajabu na hivyo kuwasiliana na watoto wengi na familia zao iwezekanavyo. Kwa hivyo, mnamo 2021, kipande cha ardhi kilinunuliwa nje ya jiji na tukapata vibali muhimu vya kuanza ujenzi. Sasa msingi umewekwa tayari. Tunamshukuru Mungu sana kwa kugusa mioyo yenu—wale ambao mmefadhili mradi hadi hatua hii na wale ambao mtafanya hivyo kwa wingi sasa. Kwa zawadi yako, utawapa watoto wasiomjua Mungu nafasi ya kumkaribia na kupokea elimu ya Kikristo. Tunaomba nia yako njema na tuna hakika kwamba hutabaki kutojali, lakini utatuunga mkono ili kukamilisha mradi huu kwa mafanikio na kutubeba katika maombi yako pia.

*Ndugu zenu na dada kutoka  Union ya Romanian*

Sabato, Marchi 1, 2025

**Somo la 9**

# Kuzaliwa kwa Mmisionari

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Hamsemi ninyi, Bado miezi minne, ndipo yaja mavuno? tazama, nawaambia, Inueni macho yenu, myatazame mashamba; ya kuwa yamekwisha kuwa meupe tayari kuvunwa" (Yohana 4:35).

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 5, pp. 182–187.

"Yesu alikuwa ameanza kubomoa ukuta unaotenganisha Wayahudi na Mataifa, na kuhubiri wokovu kwa ulimwengu. Ingawa alikuwa Myahudi, alichangamana kabisa na Wasamaria, akionyesha kwamba desturi za Kifarisayo za taifa lake si kitu. " — *The Desire of Ages,* p. 193.

## 1. MAISHA MAPYA, VIPAUMBELE VIPYA — 2/23 (Jpil)

**a. Baada ya kumtambua Yesu kuwa Masihi, mwanamke Msamaria alifanya nini mara moja? Yohana 4:28, 29.**

"Yule mwanamke alikuwa amejazwa na furaha kadiri alivyosikiliza maneno ya Kristo. Ufunuo wa ajabu ulikuwa kama unampa nguvu za ziada. Akiacha mtungi wake wa maji, alirudi mjini, kuwapelekea wengine ujumbe. Yesu alijua ni kwa nini yule mwanamke alikuwa ameenda. Kwa kuacha mtungi wake alitamka pasipo kukosea matokeo ya maneno yale yale ya Yesu. Ilikuwa ni hamu ya moyo wake kupata maji ya uzima; na alisahau hata lengo la safari yake ya kisimani, alisahau ile kiu ya Mwokozi, ambayo alikuwa amekusudia kuifanyia kazi. Akiwa na moyo unaotiririka furaha, aliharakisha njiani, kuwajulisha wengine nuru ya thamani aliyokuwa amepokea." — *The Desire of Ages,* p. 191.

**b. Wakaaji wa Sikari walifanya nini waliposikia ushuhuda wa wenyeji wenzao? Yohana 4:30.**

"[Maneno ya mwanamke huyo]yaligusa mioyo yao. Uso wake ulikuwa na mwonekano mpya, badiliko la mwonekano wake wote. Walikuwa na hamu ya kumwona Yesu. " — Ibid.

## 2. MAVUNO NA WAVUNAJI 2/24 (Jtat)

**a. Yesu alipowaona wenyeji wa Sikari wakija, aliwaambia nini wanafunzi Wake? Yohana 4:35–38.**

”Avunaye hupokea mshahara, na kukusanya matunda kwa uzima wa milele, ili yeye apandaye na yeye avunaye wapate kufurahi pamoja. Kwa maana hapo neno hilo huwa kweli, Mmoja hupanda akavuna mwingine.” Hapa Yesu anaelekeza kwa huduma takatifu ambayo Mungu anaitaka kwa wale walioipokea injili. Wanapaswa wawe mawakala wake walio hai. Anahitaji huduma yao binafsi. Na ikiwa tunapanda au kuvuna, tunafanya kazi kwa ajili ya Mungu. Mmoja anatawanya mbegu; mwingine anakusanya mavuno; na wote mpandaji na mvunaji wanapokea ujira. Wanafurahia pamoja katika ujira wa kazi yao. ” — *The Desire of Ages*, pp. 191, 192.

**b. Je, matokeo ya ushuhuda wa mwanamke kuhusu Kristo yalikuwa nini—na tunaweza kujifunza nini kutokana na matokeo ambayo ulikuwa nayo? Yohana 4:39.**

“Tunapounganishwa na Kristo, tunakuwa na nia ya Kristo. Usafi na upendo hung’aa katika tabia, upole na ukweli hutawala maisha. kielelezo cha uso unabadilishwa. Kristo akikaa ndani ya nafsi anatoa nguvu ya kubadilisha, na sura ya nje inashuhudia amani na furaha inayotawala ndani. Tunakunywa katika upendo wa Kristo, kama vile tawi linavyochota lishe kutoka kwa mzabibu. Ikiwa tumepandikizwa katika Kristo, ikiwa nyuzi kwa nyuzi tumeunganishwa na Mzabibu Hai, tutatoa ushahidi wa ukweli kwa kuzaa vishada vya matunda hai. Ikiwa tumeunganishwa na Nuru, tutakuwa mikondo ya nuru, na kwa maneno na matendo yetu tutaangazia nuru kwa ulimwengu. . . .

“Kwa kutazama tunapaswa kubadilishwa; na tunapotafakari juu ya ukamilifu wa Kielelezo cha Mungu, tutatamani kugeuzwa kikamilifu, na kufanywa upya katika sura ya usafi Wake. Ni kwa imani katika Mwana wa Mungu kwamba mabadiliko hufanyika katika tabia, na mtoto wa ghadhabu anakuwa mtoto wa Mungu. Anapita kutoka mautini kuingia uzimani; anakuwa wa kiroho na kutambua mambo ya kiroho. Hekima ya Mungu hutia nuru akili yake, naye huona mambo ya ajabu katika sheria yake. Mwanadamu anapoongoka na ukweli, kazi ya kubadilisha tabia inaendelea.” — *Selected Messages,* bk. 1, pp. 337, 338.

## 3. UWEPO WA YESU HUKO SAMARIA 2/25 (Jnne)

**a. Wasamaria walimwomba Yesu ombi gani — na kwa nini? Yohana 4:40.**

---

**b. Elezea matokeo ya wakati wa Kristo huko Samaria. Yohana 4:41.**

---

---

"Katika maneno yaliyotamkwa kwa mwanamke yule pale kisimani, mbegu njema ilikuwa imepandwa, na mavuno yalipokewa kwa haraka kiasi gani! Wasamaria walikuja na kumsikiliza Yesu, kumwamini. Wakikusanyika kwake pale kisimani, walimwuliza maswali, na wakapokea kwa hamu ufafanuzi wake wa mambo mengi ambayo yalikuwa yamejificha kwao. Kadiri walivyosikiliza, mashaka yao yalitoweka. Walikuwa kama watu walio katika giza kuu la usiku wanaokutana na mionzi ya nuru ya ghafla hadi wakauona mchana. Lakini hawakutosheka na mkutano huu mfupi. Walitamani kusikia zaidi, na kuwafanya rafiki zao nao wamsikilize huyu mwalimu wa ajabu. Walimwalika aingie katika mji wao, na kumsihi abaki pamoja nao. Alibaki pale Samaria kwa siku mbili, na wengine wengi walimwamini. " — *The Desire of Ages,* p. 192.

"Kristo alimfunua Mungu kwa wanafunzi wake kwa njia ambayo ilifanya mioyoni mwao kazi ya pekee, kama vile ambavyo amekuwa akituhimiza kwa muda mrefu tumruhusu afanye ndani ya mioyo yetu. Kuna wengi ambao, kwa kukaa sana juu ya nadharia, wamepoteza uwezo wa kuishi wa mfano wa Mwokozi. Wamepoteza kumwona kama mfanyakazi mnyenyekevu, anayejinyima. Wanachohitaji ni kumtazama Yesu. Kila siku tunahitaji ufunuo mpya wa uwepo wake." — *Refiecting Christ*, p. 302.

**c. Wasamaria wengi walitangaza nini baada ya kumkubali Yesu kuwa Masihi? Yohana 4:42.**

---

---

"Mafarisayo walidharau urahisi wa Yesu. Walipuuza miujiza yake, na kumdai ishara ya kuonyesha kama alikuwa Mwana wa Mungu. Lakini Wasamaria hawakudai kupewa ishara yoyote, na wala Yesu hakufanya mwujiza miongoni mwao, ila tu kumfunulia yule mwanamke siri za maisha yake pale kisimani. Lakini wengi walimwamini. Wakiwa katika furaha yao mpya walimwambia yule mwanamke, "Sasa tunaamini, wala si kwa sababu ya maneno yako tu; maana sisi tumesikia wenyewe, tena twajua ya kuwa hakika huyu ndiye Mwokozi wa ulimwengu." — *The Desire of Ages*, pp. 192, 193.

**a. Wasamaria walitegemeza imani yao katika unabii gani katika Masihi aliyeahidiwa? Mwanzo 49:10.**

---

---

"Wasamaria waliamini kwamba Masihi angekuja kama Mkombozi, si kwa ajili ya Wayahudi tu, bali kwa ajili ya ulimwengu. Roho Mtakatifu kupitia Musa alikuwa amemtabiri Masihi kama nabii atakayetumwa na Mungu. Kupitia Yakobo ilikuwa imesemwa kwamba watu watakusanywa kwake Masihi; na kupitia kwa Ibrahimu, ilisemwa kwamba katika Masihi mataifa yote watabarikiwa. Kutokana na maandiko haya watu wa Samaria waliweka imani yao kwa Masihi. Hali ya kwamba Wayahudi walikuwa wametafsiri vibaya unabii wa baada ya huo, wakiuhusisha utukufu wa kuja kwa Kristo mara ya pili katika kule kuja kwake mara ya kwanza, ilikuwa imesababisha Wasamaria kukataa maandiko matakatifu yote isipokuwa yale yaliyotolewa na Musa tu. Lakini wakati Yesu alipofagilia mbali hizi tafsiri potofu, wengi walikubali unabii wa baadaye na maneno ya Kristo mwenyewe kuhusu ufalme wa Mungu." — *The Desire of Ages*, p. 193.

**b. Tunaweza kujifunza nini leo kutokana na ukweli kwamba Wasamaria walikuwa wazi kwa njia ya ajabu kwa ukweli? Mhubiri 11:4,5.**

---

---

"Ulimwenguni kote wanaume na wanawake wanatazama mbinguni kwa shauku. Maombi na machozi na maswali hupanda kutoka kwa roho zinazotamani nuru, neema, na Roho Mtakatifu. Wengi wako kwenye ukingo wa ufalme, wakingoja tu kukusanywa." — *The Acts of the Apostles*, p. 109.

**c. Je, watu wanakuwaje wanapompokea Kristo kweli kweli? Toa mifano. Marko 5:18–20; 7:31–37.**

---

---

"[Roho wa Kristo] atayaendeleza ndani ya mtu yale yote yatakayoifanya tabia kuwa njema na kuiinua hali ya mwanadamu. Atamjenga mtu kwa ajili ya utukufu wa Mungu katika mwili na nafsi na roho...... Na nafsi zile ambazo zimeshushwa na kuwa vitendea-kazi vya Shetani bado zinabadilishwa kwa nguvu ya Kristo na kufanywa kuwa wajumbe wa haki, na Mwana wa Mungu humtuma mtu kama huyo akimwambia, Nenda ukasimulie "ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu." — *The Desire of Ages*, p. 341.

## 5. WAMISIONARI WA KIKRISTO — 2/27 (Alham)

a. Tunajifunza mambo gani kutoka kwa mwanamke Msamaria? 1Yohana 1:1–3; 2Wakorintho 5:14 (sehemu ya kwanza).

---

“Muda mfupi baada ya kumpata Mwokozi mwanamke Msamaria aliwaleta wengine kwake. Alijipambanua kuwa na uwezo wa umishonari kuliko hata wanafunzi wenyewe wa Yesu. Wanafunzi wale hawakuona chochote pale Samaria kilichoonyesha kuvutia kazi ya utume. Mawazo yao yalikuwa yamekazwa kwa kazi kuu ambayo ingefanyika siku za usoni. Hawakuona kwamba katika maeneo ya pale pale tu panapowazunguka kulikuwa na mavuno ya kukusanywa. Lakini kupitia mwanamke ambaye walimdharau, wakazi wa mji wote waliletwa kumsikia Mwokozi. Mara tu aliipeleka nuru kwa watu wa nchi yake.

“Mwanamke huyu anawakilisha utendaji wa imani katika Kristo. Kila mwanafunzi wa kweli anazaliwa ili kuingia katika ufalme wa Mungu kama mmishonari. Yeye anayekunywa kutoka katika maji ya uzima anakuwa chemchemi ya uzima. Anayepokea huwa mtoaji. Neema ya Kristo katika nafsi ya mtu ni kama chemchemi jangwani, inayotoa maji ili kuwaburudisha watu wote, na kuwafanya walio karibu kuangamia kuwa na hamu ya kunywa katika maji ya uzima. ” — *The Desire of Ages*, p. 195.

b. Je, uzoefu huu unatutia moyo jinsi gani leo? Mhubiri 11:6.

---

“Hatuna haja ya kwenda nchi za nje ili kuwa wamishonari wa Mungu. Karibu yetu kuna mashamba „yameiva tayari kuvunwa,” kwa yeyote anayekusanya „matunda kwa ajili ya uzima wa milele.” Mungu anatoa wito kwa wengi Battle Creek ambao wanakufa kwa uvivu wa kiroho kwenda mahali ambapo nguvu yao inahitajika kwa kazi Yake. Ondokeni Battle Creek, hata ikiwa inahitaji kujitoa kifedha. Nendeni mahali pengine kuwa baraka kwa wengine. Nendeni mahali ambapo mnaweza kuimarisha kanisa dhaifu. Tumieni uwezo/nguvu ambazo Mungu amewapatia. ” — *Testimonies for the Church*, vol. 5, p. 187.

## 6. MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI — 2/28 (Ijumaa)

1. Mwanamke alifanya nini alipomwona Yesu kama Mwokozi pekee?
2. Eleza nini maana ya mashamba kuwa meupe tayari kwa mavuno.
3. Je Yesu alikaa na Wasamaria kwa siku ngapi?
4. Wasamaria walitoa ushuhuda gani kuhusu Yesu?
5. Ni nini kinatokea kwa watu mara tu wanapompokea Yesu maishani mwao?

Sabato, Marchi 8, 2025

**Somo la 10**

# Yesu na Mwana wa Diwani

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu. Amina" (Waefeso 3:20, 21).

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 9, pp. 107, 108, 164–166.

"Sio kwa sababu tunaona au kuhisi kwamba Mungu anatusikia ndio Tunapaswa tuamini katika ahadi zake. Tunapokuja kwake kwa imani, kila ombi linaingia katika moyo wa Mungu. Wakati tunapokuwa tumeomba mbaraka wake, tunatakiwa tuamini kwamba tunaupokea, na kumshukuru kwamba tumeupata. Halafu tunatakiwa tuendelee na majukumu yetu, tukiwa na hakika kwamba mbaraka ule utadhihirishwa wakati ule tunapouhitaji zaidi. " — *The Desire of Ages,* p. 200.

## 1. KUVUTA USIKIVU

3/2 (Jpil)

**a. Baada ya kukaa siku mbili pamoja na Wasamaria, Yesu alienda wapi—na ni nani aliyevutwa na habari hizi? Yohana 4:43–46.**

"Habari kwamba Kristo alikuwa amerudi Kana zilisambaa kote Galilaya, zikileta matumaini kwa wenye shida na wanaoteseka. Kule Kapernaumu habari hizo zilivuta usikivu wa Myahudi aliyekuwa diwani katika utumishi wa mfalme" — *The Desire of Ages*, p. 196.

**b. Kwa nini ofisa alienda kumwona Yesu? Yohana 4:47.**

"Kijana wa mtumshi huyo alikuwa anaumwa ugonjwa ambao ulionekana kama usiotibika. Matabibu walikuwa wameshindwa na kumwacha afe; lakini pindi baba yule aliposikia habari za Yesu, aliamua kutafuta msaada kwake." — *Ibid.*, p.197.

## 2. DALILI YA MASHAKA 3/3 (Jtat)

**a. Eleza jinsi Kristo alivyofunua huzuni ya ndani ya moyo wa yule diwani aliyemtafuta kumponya mwanawe huko Kapernaumu. Yohana 4:48.**

---

---

“Mtoto alikuwa katika hali mbaya sana, na, iliogopesha kwamba baba yule asingerudi na kumkuta bado yuko hai; lakini mtumishi yule wa mfalme aliona kwamba lazima alifikishe kwa Yesu jambo hilo yeye mwenyewe. Alitumaini kwamba huenda ombi linalowasilishwa na baba lingeweza kuamsha huruma ya Tabibu Mkuu.

“Alipofika Kana alikuta umati mkubwa ukiwa umemzunguka Yesu. Akiwa na moyo wenye dukuduku alipenya hadi mahali alipokuwa Mwokozi. Imani yake ilipungua alipomwona mtu aliyevaa nguo za kawaida, mwenye mavumbi na uchovu wa safari. Alipata mashaka ikiwa kweli Mtu huyu angefanya kile ambacho amekuja kuomba; lakini bado alipata nafasi ya kuongea na Yesu, akamwambia sababu ya ujio wake kwake, na kumsihi Mwokozi aongozane naye kwenda nyumbani kwake. Lakini tayari huzuni ilikuwa inajulikana kwa Yesu. Diwani yule alipokuwa hajaondoka nyumbani kwake, Mwokozi alikuwa ameshaona shida yake.

“Lakini alijua pia kwamba baba yule alikuwa, mawazoni mwake, ameweka masharti kuhusu imani yake kwa Yesu. Ikiwa ombi lake lisingefanyiwa kazi, asingempokea Yesu kama Masihi……

“Licha ya ushahidi wote kwamba Yesu alikuwa ni Kristo, yule aliyeleta ombi alikuwa ameazimia kuifanya imani yake iwe ya sharti la ombi lake kufanyiwa kazi. ” — *The Desire of Ages*, pp. 197, 198.

**b. Tunaposhawishiwa kutafuta ishara, tunapaswa kukumbuka nini? Mathayo 12:38, 39.**

---

---

“Yesu aliumia kwa sababu watu wake mwenyewe, ambao walikabidhiwa Maneno Matakatifu, wangeshindwa kuisikia sauti ya Mungu akiongea nao katika Mwana wake. ” — *Ibid.*, p. 198.

“Watu wanataka ishara, kama katika siku za Kristo. Kisha Bwana akawaambia kwamba wasipewe ishara yoyote. Ishara inayopaswa kudhihirika sasa na daima ni utendaji kazi wa Roho Mtakatifu juu ya akili ya mwalimu, kulifanya Neno liwe la kuvutia kadiri inavyowezekana. Neno la Mungu si nadharia mfu, kavu, bali ni roho na uzima. Shetani hangependa kitu bora zaidi kuliko kuwaondoa watu kutoka kwa Neno, kutafuta na kutarajia kitu nje ya Neno kuwafanya wajisikie.”— *Selected Messages,* bk. 2, p. 95.

**a. Elezea tofauti kati ya Wayahudi na Wasamaria kuhusiana na imani yao katika Yesu. Marko 6:2–6; Yohana 4:40–42.**

---

---

“Mafarisayo walitaka sana kuthibitisha kwamba Kristo ni mdanganyifu! Jinsi walivyotazama kila neno Lake, wakitafuta kupotosha na kutafsiri vibaya maneno Yake yote! Kiburi na chuki na shauku vilifunga kila njia ya nafsi dhidi ya ushuhuda wa Mwana wa Mungu. Alipokemea uovu wao waziwazi na kutangaza kwamba matendo yao yamewathibitisha kuwa watoto wa Shetani, kwa hasira waliyatupilia mbali mashitaka hayo, wakisema, ‘Je, hatusemi kweli kwamba wewe ni Msamaria, na kwamba una pepo?’ ” — *Selected Messages,* bk. 1, p. 70.

“Mwokozi alilinganisha huku kutoamini ambako kuna maswali na imani ile rahisi ya Wasamaria, ambao hawakutaka mwujiza wala ishara. Neno lake, ushahidi uliopo siku zote wa uungu wake, lilikuwa na nguvu ya kushawishi ambayo iliifikia mioyo yao.” — *The Desire of Ages,* p. 198.

“Ingawa [Yesu] alikuwa Myahudi, Alichangamana kwa uhuru na Wasamaria, akipuuza desturi za Kifarisayo za Wayahudi kuhusu watu hao waliodharauliwa. Alilala chini ya dari zao, akala mezani mwao, na kufundisha katika mitaa yao.” — *The Acts of the Apostles,* p. 19.

**b. Elezea uzoefu wa wengi ambao wamezungumza ukweli wa sasa kwa watu wanaodai kuwa watu wa Mungu katika zama zote. Yeremia 20:8–11.**

---

---

“Mabishano yote yaliyohimizwa dhidi ya Kristo yaliwekwa katika uwongo. Ndivyo ilivyokuwa katika kisa cha Stefano, na cha Paulo. Lakini kauli dhaifu na zisizotegemewa zilizotolewa upande mbaya zilikuwa na mvuto, kwa sababu kulikuwa na wengi ambao mioyo yao haikutakaswa, ambao walitamani kauli hizo ziwe za kweli. Watu hao huwa na shauku ya kudumu juu ya kosa lolote linalofikiriwa kuwa au kosa katika wale wanaozungumza nao ukweli usiopendeza.

“Haipaswi kutushangaza wakati dhana ovu zinapochukuliwa kwa pupa kuwa mambo yasiyo na shaka na wale ambao wana hamu ya uwongo. Wapinzani wa Kristo walichanganyikiwa tena na tena na kunyamazishwa na hekima ya maneno yake; lakini bado walisikiliza kila uvumi kwa hamu, na wakapata kisingizio cha kumhoji tena kwa maswali yanayopingana.” — *Selected Messages,* bk. 1, pp. 70, 71.

## 4. OMBI KWA UNYENYEKEVU 3/5 (Jtan)

**a. Wakati imani ya diwani huyo ilipomshika Kristo, alirudiaje ombi lake? Yohana 4:49.**

"Kama kumlika kwa nuru, maneno ya Mwokozi kwa diwani yaliuweka wazi moyo wake. Aliona kwamba misukumo yake ya kumtafuta Yesu ilikuwa ya ubinafsi. Imani yake isiyo na msimamo ilionekana kwake kama tabia yake kweli kweli. Katika shida aliyokuwa nayo alitambua kwamba mashaka yake yangeweza kugharimu maisha ya mwanawe. Alijua kwamba alikuwa mbele yake Yeye aliyeweza kusoma mawazo, na ambaye kwake mambo yote yalikuwa yanawezekana. Katika maumivu ya kuomba alisema, "Bwana, ushuke asijakufa mtoto wangu." Imani yake ilimshikilia Kristo kama alivyofanya Yakobo, wakati, alipokuwa akipambana mieleka na Malaika, alipolia akisema, „Sikuachi, usiponibariki." Mwanzo 32:26. — *The Desire of Ages,* p. 198.

**b. Je, tunapaswa kujifunza nini kutokana na kile Yesu alifanya badala ya kwenda nyumbani kwa yule diwani? Yohana 4:50.**

"Yesu alikuwa na zawadi ya kutoa iliyo kubwa zaidi. Alitaka, si kuponya tu mtoto yule, bali pia kumfanya diwani na nyumba yake kuwa washiriki wa mibaraka ya wokovu, na kuwasha nuru pale Kapernaumu, ambapo baada ya muda mfupi pangekuwa sehemu ya kazi yake. Lakini lazima diwani huyu afanikishe hitaji lake kabla ya kutamani neema ya Yesu. Mtu huyu mkuu aliwakilisha watu wengi wa taifa lake. Walivutiwa na Yesu kwa sababu za manufaa binafsi. Walitarajia kupata faida fulani maalum kupitia uwezo wake, na waliweka imani yao katika kupewa mema ya ulimwengu; lakini hawakuwa wanajua kuhusu ugonjwa wao wa kiroho, na hawakuona hitaji la neema ya mbinguni.. . . .

"Yesu hawezi kuondokana na nafsi inayomng'ang'ania, ikiomba kwa ajili ya hitaji kubwa. Alisema, "Enenda; mwanao yu hai." Yule diwani aliondoka kwa Yesu kwa amani na furaha kwa kiasi ambacho hakupata kujua kabla. Si tu kwamba alijua mwana wake alikuwa amepona, bali pia kwa ujasiri mkubwa alimwamini Kristo kama Mkombozi. " — *Ibid.,* pp. 198, 199.

"Sisi sote tunatamani majibu ya haraka na ya moja kwa moja kwa maombi yetu, na tunajaribiwa kukata tamaa jibu linapochelewa au kuja kwa namna ambayo haijatazamwa. Lakini Mungu ni mwenye hekima sana na ni mwema kujibu maombi yetu sikuzote kwa wakati na kwa jinsi tunavyotamani. Atafanya zaidi na bora zaidi kwa ajili yetu kuliko kutimiza matakwa yetu yote. Haya mambo ambayo imani hujaribu ni kwa manufaa yetu." — *The Ministry of Healing*, pp. 230, 231.

## 5. TIBA NA WOKOVU — 3/6 (Alhamis)

**a. Je, Yesu alimponya mtoto wa diwani kwa namna gani? Yohana 4:51–53. Je, hii inakumbusha ukweli gani? Waefeso 3:20, 21.**

---

---

"Katika muda ule ule imani ya baba huyo ilipopewa uhakika kwamba, "Mwanao yu hai," upendo wa kimbingu ulimgusa mtoto aliyekuwa kifoni." — *The Desire of Ages*, p.199.

"Katika saa ile ile waangalizi waliokuwa kando ya yule mtoto aliye karibu kufa kule nyumbani Kapernaumu waliona badiliko la ghafla na la ajabu. Uvuli wa mauti uliondolewa katika uso wa mgonjwa. Kuhisi homa kulitoweka na mahali pake kukawa na mwonekano wa afya njema. Macho maangavu yanayoonyesha uwezo mzuri wa akili, na nguvu, vilirejea kwa mgonjwa. Hakuna dalili za ugonjwa zilizoendelea kuonekana kwa mtoto yule. Mwili wake uliokuwa wa moto ulikuwa umelainika na kuwa na unyevunyevu, na alizama katika usingizi. Homa ilimwacha katika hali ya joto la mchana. Watu wa nyumba ile walishangazwa, na wakawa na furaha kuu. "—Ibid.

**b. Yesu anamjibuje mtu yeyote anayeomba msaada? Mathayo 11:28–30.**

---

"Yesu hawezi kuondokana na nafsi inayomng'ang'ania, ikiomba kwa ajili ya hitaji kubwa." — *Ibid.*, p. 198.

"Je, unahisi kwamba kwa sababu wewe ni mwenye dhambi huwezi kutumaini kupokea baraka kutoka kwa Mungu? Kumbuka kwamba Kristo alikuja ulimwenguni kuokoa wenye dhambi. Hatuna kitu cha kutupendekeza kwa Mungu; ombi ambalo tunaweza kuhimiza sasa na siku zote ni hali yetu isiyo na msaada kabisa, ambayo inafanya uwezo wake wa ukombozi kuwa wa lazima. Tukiacha utegemezi wote wa kibinafsi, tunaweza kutazama msalaba wa Kalvari na kusema: "Sina cha mkononi; Naja msalabani.' " — *The Ministry of Healing,* p. 65.

## 6. MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI — 3/7 (Fri)

1. Kwa nini manabii kwa ujumla hawapokelewi vyema katika nchi zao?
2. Ni maneno gani ya mtukufu huyo yalidhihirisha kutokuamini kwake?
3. Je Kristo aliitikiaje kutokuamini kwa watu?
4. Ni nani walioonyesha imani kubwa zaidi katika Yesu—Wayahudi au Wasio Wayahudi?
5. Yesu anaahidi nini kwa wote wanaokubali mwaliko wake?

Sabato, Marchi 15, 2025

**Somo la 11**

# Yesu na yule aliyepooza wa Bethzatha

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Lakini Yesu akawajibu, Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi" (Yohana 5:17).

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 1, pp. 560–567.

"Kazi ya Kristo katika kumponya mgonjwa yule ilikuwa inakubaliana na sheria. Iliitukuza Sabato. " — *The Desire of Ages,* p. 207.

## 1. AMAZI AKIZA

Kuwa Mbere
09 Werurwe

**a. Wasiojiweza wengi walienda Yerusalemu kwa kusudi gani? Yohana 5:2,3.**

---

---

**b. Je, watu walikuwa na imani gani kuhusu birika la Bethzatha? Yohana 5:4.**

---

"Katika nyakati fulani maji ya birika hili yalikuwa yakitibuliwa, na ilikuwa inaamika kote kwamba hali hii ilikuwa inasababishwa na nguvu isiyo ya kibinadamu, na ya kwamba yeyote aliyekuwa wa kwanza kurukia birikani baada ya maji kuvurugwa au kusukwasukwa alipona ugonjwa wowote aliokuwa nao. Mamia ya wagonjwa walitembelea mahali pale; lakini umati mkubwa ulikuwepo baada hasa ya maji kuvurugwa ambapo walikimbia mbele, wakiwakanyaga wanaume, wanawake, na watoto, waliokuwa dhaifu zaidi kuliko wao. Wengi hawakuweza kusogea karibu na kingo za birika. Wengi waliokuwa wamefanikiwa kulifikia birika hili walifia pale kwenye kingo zake. Vibanda vilikuwa vimejengwa mahali pale, ili kwamba wagonjwa wahifadhiwe dhidi ya joto la mchana na baridi ya usiku. Walikuwepo wengi waliosubiri usiku mzima katika matao haya, wakisogea karibu katika ukingo wa birika siku baada ya siku, wakitafuta pasipo mafanikio kupona. " — *The Desire of Ages,* p. 201.

**c. Uhusiano kati ya Yesu na mtu mmoja kwenye birika yalianzaje? Yohana 5:5–7.**

---

**a. Je, ni kazi gani isiyowezekana ya kibinadamu ambayo Yesu aliamuru yule aliyepooza afanye—na matokeo yalikuwa nini? Yohana 5:8, 9 (sehemu ya kwanza).**

---

---

"Yesu hamwulizi mgonjwa huyu kufanya tendo la kuwa na imani kwa Yesu. Anamwambia tu kwamba, "Simama, jitwike godoro lako, uende." Imani ya mtu yule inalishikilia lile neno. Kila neva na msuli vilipata uzima upya, na uwezo wa afya ulikuja katika miguu yake iliyolemaa. Pasipo kuhoji aliweka utashi wake katika kutii maelekezo ya Kristo, na misuli yake yote iliitika kuufuata utashi ule. Alijitegemeza kwenye miguu yake, akajikuta yuko imara.

"Yesu hakuwa amempatia uhakika wa msaada wa uungu. Yule mtu angeweza kuacha kwa mashaka, na angepoteza nafasi ya kupona. Lakini aliamini neno la Kristo, na kwa kuliweka katika vitendo alipata nguvu." — *The Desire of Ages,* pp. 202, 203.

**b. Watu waliojitenga na Kristo wanajikuta katika hali gani ya kiroho? Isaya 1:5, 6; Warumi 7:24.**

---

"Kwa sababu ya dhambi tunatengwa na maisha ya Mungu. Nafsi zetu zimelemazwa. Sisi wenyewe hatuwezi tena kuishi maisha matakatifu kama ambavyo mtu yule mlemavu hakuwa na uwezo wa kutembea. Wapo wengi wanaotambua kwamba hawajiwezei lolote, na ambao wanatamani maisha yale ya kiroho yatakayowaleta katika kupatana na Mungu" — Ibid., p. 203.

**c. Je, ni tiba gani pekee ya hali kama hiyo? Matendo 9:34.**

---

"Mwokozi anasihi kwa damu yake iliyowanunua, akisema kwa huruma isiyosemekana, „Wataka kuwa mzima?" Anakusihi usimame katika afya na amani. Usisubiri mpaka utakapojisikia kama umepona. Amini neno lake, na itatendeka. Weka utashi wako upande wa Kristo. Hiari kumtumikia, na kwa kufanyia kazi neno lake utapata nguvu. Hata kama kuna mambo gani ya uovu, mateso makubwa ya mwili na roho, Kristo anaweza na anatamani kuokoa. Ataweka uzima katika nafsi ile ambayo ni mojawapo ya "wafu kwa sababu ya makosa na dhambi." Waefeso 2:1. Atamweka huru mateka aliyeshikiliwa na udhaifu na kukosa furaha na minyororo ya dhambi. "—Ibid.

## 3. KUTEMBEA KATIKA UPYA WA MAISHA 3/11 (Jnne)

a. Kristo anatusaidiaje kushinda? Waefeso 2:1–6.

“Mwanadamu ameelekezwa kufuata matakwa ya Shetani, na hawezi kufanikiwa kumpinga adui huyu mbaya sana isipokuwa Kristo, mshindi hodari, akae ndani yake, akiongoza tamaa zake, na kumtia nguvu. Shetani anajua vizuri kuliko watuwa Mungu nguvu ambayo wanaweza kuwa nayo juu yake wakimuelekea na kumfuata Kristo.Wanapoomba kwa unyenyekevu kwa msaidizi mwenye nguvu kwa ajili ya msaada, hata muumini dhaifu kabisa wa ukweli, akimtegemea Kristo kikamilifu, anaweza kufanikiwa kumshinda Shetani na jeshi lake lote. ” — *Testimonies for the Church*, vol. 1, p. 341.

“Ni lazima tujifunze kwa Kristo. Ni lazima tujue Yeye ni nini kwa wale aliowakomboa. Ni lazima tutambue kwamba kwa njia ya kumwamini Yeye ni fursa yetu kuwa washirika wa asili ya kimungu, na hivyo kuepuka uharibifu ulio duniani kwa njia ya tamaa. Kisha tunatakaswa kutoka kwa dhambi zote, kasoro zote za tabia. Hatuhitaji kuwa na tabia moja ya dhambi.....

“Tunaposhiriki asili ya kimungu, mielekeo ya kurithi na iliyokuzwa ya kufanya vibaya hukatiliwa mbali na tabia hiyo, na tunafanywa kuwa nguvu hai kwa ajili ya wema. Kila mara tukijifunza juu ya Mwalimu wa Mungu, tukishiriki asili yake kila siku, tunashirikiana na Mungu katika kuyashinda majaribu ya Shetani. Mungu anafanya kazi, na mwanadamu anafanya kazi, ili mtu awe mmoja na Kristo kama vile Kristo alivyo mmoja na Mungu. Kisha tunaketi pamoja na Kristo katika ulimwengu wa roho. Akili inapumzika na amani na uhakika ndani ya Yesu.” — *The Review and Herald,* April 24, 1900.

b. Elezea amani inayokuja kwa nguvu kutoka kwa Kristo. Warumi 8:3–6.

“Kila mtoto huishi kwa uhai wa baba yake. Kama ninyi ni watoto wa Mungu, - mliozaliwa kwa Roho wake, - mnaishi kwa uzima wa Mungu. Katika Kristo “unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili” na uhai wa Yesu unadhihirishwa “katika miili yetu ipatikanayo na mauti” (2 Wakorintho 4:11). Uhai ule ukiwa ndani yenu utafanyiza tabia ile ile na kuonesha matendo yale yale kama ulivyofanya ndani yake. Hivyo mtapatana na kila agizo la sheria yake; kwani “sheria ya Bwana ni kamilifu, huiburudisha nafsi.” Zaburi 19:7. Kwa njia ya upendo “maagizo ya torati” yata“timizw(a) ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho.” Warumi 8:4.” — *Thoughts From the Mount of Blessing*, p. 78.

## 4. HASIRA YA MAFARISAYO 3/12 (Jtan)

**a. Kwa kupuuza baraka aliyopewa yule aliyepooza, kwa nini Mafarisayo walikasirika? Yohana 5:9 (sehemu ya mwisho), 10.**

---

[Wakati yule mlemavu wa kupooza]"Alipokuwa akitembea haraka kwa nguvu na hatua za kupona, alimsifu Mungu na kufurahia nguvu zake mpya alizopata, alikutana na Mafarisayo kadhaa, na akawaambia haraka kuhusu kupona kwake. Alishangazwa kwa jinsi ambavyo hawakufurahishwa na kisa kile walichokuwa wanasikiliza.

"Wakiwa wameinamisha nyuso zao waliingilia na kumkatiza, wakimwuliza kwamba ni kwa nini anabeba godoro lake siku ya Sabato. Walimkumbusha kwa msisitizo kwamba haikuruhusiwa kubeba mizigo katika siku ya Bwana. Katika furaha yake mtu yule alikuwa amesahau kwamba ilikuwa siku ya Sabato; lakini hakuhisi hatia maana alitii amri yake Yeye aliyekuwa na nguvu namna ile kutoka kwa Mungu. Alijibu kwa kujiamini, "Yeye aliyenifanya kuwa mzima ndiye aliyeniambia, Jitwike godoro lako, uende." Walimwuliza kuhusu huyo aliyefanya hivyo, lakini hakuweza kueleza. Wakuu hawa walijua kwamba yupo Mmoja tu aliyekuwa ameonyesha uwezo wa kutenda miujiza; lakini walitaka wapate ushahidi wa moja kwa moja kwamba alikuwa ni Yesu, ili wamwone kwamba ana hatia ya kuvunja Sabato. Katika hukumu yao ni kwamba alikuwa amekiuka si tu kwa kuponya mtu siku ya Sabato, bali pia kwa kuacha kuheshimu kitakatifu kwa kumtaka mtu yule kubeba godoro lake. " — *The Desire of Ages,* pp. 203, 204.

**b. Je, Wayahudi walikuwa wamefanya nini kuhusu Sabato? Mathayo 23:4.**

---

"Wayahudi walikuwa wamepotosha sheria kiasi cha kuifanya kuwa kongwa la utumwa. Matakwa yao yasiyo maana yalikuwa yamekuwa kama mithali katika mataifa mengine. Hasa hasa Sabato ilikuwa imewekewa namna za makatazo yasiyo na maana. Kwao haikuwa siku ya furaha, takatifu ya Bwana, na ya heshima. Waandishi na Mafarisayo walikuwa wameyafanya maadhimisho ya Sabato kuwa mzigo usiovumilika. Myahudi hakuruhusiwa kuwasha moto wala kuwasha mshumaa. Kama matokeo yake watu waliwategemea Wamataifa kwa ajili ya huduma nyingi ambazo wasingeweza kuzifanya wao wanyewe kwa kuwa taratibu zilikataza. Hawakuona kwamba kuajiri watu wengine kufanya vitendo vilivyodhaniwa kuwa dhambi ilikuwa ni kutenda dhambi sawasawa kama vile walikuwa wamevifanya wao wenyewe. Walifikiri kwamba wokovu ulikuwa kwa ajili ya Wayahudi tu, na kwamba hali ya watu wengine, ambao tayari hawana matumaini, isingefanywa kuwa mbaya zaidi. Lakini Mungu hakutoa amri ambayo haiwezi kutiiwa na watu wote. Sheria zake haziruhusu kuwa na vizuizi visivyo na sababu au vya ubinafsi. " — *Ibid.*, p. 204.

## 5. SABATO NA LENGO LAKE — 3/13 (Alhamis)

**a. Je, Yesu alihusianisha vipi sheria ya Mungu na Sabato? Isaya 42:21.**

---

"Yesu alikuwa amekuja „kuitukuza sheria, na kuiadhimisha." Asingeweza kupunguza nafasi yake, bali kuiinua. Alikuwa amekuja kuiweka huru Sabato mbali na masharti yaliyokuwa yameifanya kuwa laana badala ya baraka." — *The Desire of Ages,* p. 206.

**b. Ni nini kinapaswa na kisichopaswa kufanywa siku ya Sabato? Kutoka 20:8–11.**

---

---

"Miongoni mwa wagonjwa waliokuwa pale birikani alichagua mwenye tatizo baya kuliko wote ili afanye kwake tendo la nguvu ya uponyaji, na kumwagiza mtu yule abebe godoro lake na kupita katika mji ili kuutangaza mwujiza mkubwa uliofanyika kwake. Jambo hili lingeibua swali kwa watu kwamba ni jambo lipi ambalo ni halali kufanywa siku ya Sabato, na lingemfungulia Yeye njia ya kukataa vizuizi vya Wayahudi kuhusu siku ya Bwana, na kumwezesha kutangaza kukataa mapokeo yao.

"Yesu alitamka kwamba kazi ya kumponya mgonjwa ilikuwa inapatana na sheria ya Sabato. Ilikuwa inapatana na kazi ya malaika za Mungu, ambao wanashuka na kupanda daima kati ya mbingu na dunia wakiwahudumia wanadamu wanaoteseka.....

"Hata mwanadamu pia anayo kazi ya kufanya katika siku hiyo. Lazima mambo muhimu ya maisha yashughulikiwe, lazima wagonjwa watunzwe, lazima mahitaji ya wahitaji yatolewe. Yeye anayepuuza kutuliza wanaoteseka siku ya Sabato hatahesabiwa kwamba hana hatia. Siku ya Mungu ya kupumzika ilifanywa kwa ajili ya mwanadamu, na matendo ya huruma yanapatana na kusudi la siku hiyo kwa ukamilifu. Mungu hapendi viumbe vyake viteseke hata kwa saa moja ya maumivu ambayo yangeweza kupozwa siku ya Sabato au siku nyingine yoyote." — *Ibid*., pp. 206, 207.

## 6. MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI — 3/14 (Ijumaa)

1. Ni imani gani ilikuwa imeenea kuhusu bwawa la Bethesda?
2. Ni kesi gani maalum iliyovutia umakini wa Kristo?
3. Je, kupooza kwetu kiroho kunaweza kuponywaje?
4. Ni nini kiliwakera sana Wayahudi kuhusu uponyaji wa kimuujiza?
5. Ni kazi gani zinazopatana na amri ya Sabato?

Sabato, March 22, 2025

**Somo la 12**

# Mamlaka ya Mwana

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Kwa maana kama vile Baba alivyo na uzima nafsini mwake; vivyo hivyo alimpa na Mwana kuwa na uzima nafsini mwake; Naye akampa amri ya kufanya hukumu pia, kwa sababu ni Mwana wa Adamu" (Yohana 5:26, 27 ).

**Inapendekezwa kusoma:** *Thoughts From the Mount of Blessing,* pp. 123–129.

"Mamlaka yangu, [Yesu] Alisema kwamba, kwa kufanya kazi ambayo mnanishtakia ni hii ya kwamba, Mimi ni Mwana wa Mungu, mmoja naye kwa hali, dhamira, na kusudi. Katika kazi zake zote za uumbaji na uhuishaji, ninashiriki pamoja naye. " — *The Desire of Ages,* p. 208.

## 1. SAWA NA MUNGU

3/16 (Jpil)

**a. Mbali na uponyaji wa mtu aliyepooza siku ya Sabato, ni kwa sababu gani nyingine Wayahudi walimchukia Yesu? Yohana 5:17, 18.**

"Yesu alidai haki sawa na Mungu....

"Taifa lote la Wayahudi walimwita Mungu Baba yao, kwa hiyo wasingechukizwa hivyo Kristo anapojionyesha kuwa katika uhusiano na Mungu kama vile walivyokuwa. Lakini walimtuhumu kwa kukufuru, kuonyesha kwamba walimwelewa kwa kudai dai hilo lililo bayana."—*The Desire of Ages*, pp. 207, 208.

**b. Kristo alifunuaje mamlaka ya amri za Mungu juu ya mapokeo ya wanadamu? Mathayo 15:1–9,13.**

"Wapinzani hawa wa Kristo hawakuwa na hoja za kubishana na ukweli ambao Yesu aliufikisha mahali pake katika dhamiri zao. Wangerejea katika desturi na mila zao tu, na hizi zilionekana dhaifu sana zikilinganishwa na hoja za Yesu zilizotoka katika neno la Mungu na mizunguko isiyokoma ya maumbile ya asili. " — Ibid., p. 208.

## 2. UMOJA NA BABA 3/17 (Jtat)

**a. Yesu alielezeaje uhusiano wake na Baba? Yohana 5:19,20.**

---

---

**b. Je, ni mamlaka na nguvu gani zinazomhusu Baba ambazo Kristo alitangaza kwamba Yeye pia anazo? Yohana 5:21–23.**

---

---

"Makuhani na wakuu walikuwa wamejiweka kuwa waamuzi wa kuihukumu kazi ya Kristo, lakini alijitangaza kuwa Yeye ndiye hakimu wao, na hakimu wa dunia yote. Ulimwengu umekabidhiwa kwa Kristo, na kupitia kwake kila mbaraka umekuja kwa wanadamu kutoka kwa Mungu. Alikuwa Mkombozi kabla ya kufanyika mwili kama alivyokuwa baada ya hapo. Muda mfupi tu baada ya kuwepo kwa dhambi kulikuwa na Mwokozi. Amewapatia watu wote nuru, na kulingana na kipimo cha nuru iliyotolewa, kila mmoja atahukumiwa. Na Yeye ambaye ametoa nuru, Yeye ambaye ameifuata roho kwa kusihi kwa upendo, akitafuta kuiokoa kutoka dhambini na kuileta katika utakatifu, Yeye ndiye mtetezi na hakimu. " — *The Desire of Ages*, p. 210.

**c. Eleza mabadiliko ya mtazamo yanayotokea tunapotambua kwamba Kristo ndiye mwamuzi wetu. Warumi 2:1–3; Mathayo 7:1.**

---

"Aliye na moyo wa kuwalaumu wengine yu mwenye kosa kubwa kuliko yule anayemshtaki; kwa maana yeye siyo tu anafanya kosa lile lile, bali anaongeza juu yake makosa ya kujivuna na kuwa na moyo wa kuwalaumu wengine.

"Kristo ndiye kipimo halisi cha tabia; na yule ajiwekaye mwenyewe kuwa kipimo cha wengine, anajiweka mahali pa Kristo. Na kwa kuwa Baba "amempa Mwana hukumu yote" (Yohana 5:22), ye yote anayethubutu kuhukumu nia na makusudi ya wengine anajinyakulia tena mamlaka yamhusuyo Mwana wa Mungu peke yake. Mahakimu hao na wakosoaji hao wanaojiweka wenyewe wanajiweka upande wa Mpinga Kristo, "ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu; akijionesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu." 2Wathesalonike 2:4"—*Thoughts From the Mount of Blessing*, pp. 125, 126.

"Sisi hatuwezi kuyasoma yaliyomo moyoni. Kwa kuwa sisi wenyewe tu wenye makosa, hatustahili kuwahukumu wengine. Wanadamu wanaweza kuhukumu kwa kulitazama umbo la nje tu. Yeye peke yake ajuaye mambo ya moyoni, ambaye ni mwenye hisani na huruma, ndiye atakayekata shauri juu ya kila mtu." — *Ibid.,* p. 124.

## 3. UHAKIKISHO WA THAMANI 3/18 (Jnne)

**a. Ni uhakikisho gani unaotolewa kwa kila muumini aliyejitoa kwa Kristo? Yohana 5:24.**

“Katika kila amri na katika kila ahadi ya neno la Mungu kuna nguvu, uzima halisi wa Mungu, ambao kwa hayo amri inaweza kutimizwa na ile ahadi. Yeye ambaye kwa imani anapokea neno anapokea uzima halisi na tabia ya Mungu.” — *Christ’s Object Lessons,* p. 38.

“Kazi kubwa inayotendwa kwa mwenye dhambi ambaye ametiwa doa na kuchafuliwa na uovu ni kazi ya kuhesabiwa haki. Na Yeye asemaye kweli amehesabiwa haki. Bwana humhesabia muumini haki ya Kristo na humtangaza kuwa mwenye haki mbele ya ulimwengu. Anahamisha dhambi zake kwa Yesu, mwakilishi wa mwenye dhambi, mbadala, na mdhamini. Juu ya Kristo anaweka uovu wa kila mtu aaminiye. ‘Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu; ili tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye’ (2 Wakorintho 5:21)....

“Ingawa kama wenye dhambi tuko chini ya hukumu ya sheria, lakini Kristo kwa utii wake uliotolewa kwa sheria, anadai kwa ajili ya nafsi iliyotubu stahili ya haki yake mwenyewe. Ili kupata haki ya Kristo, ni muhimu kwa mwenye dhambi kujua ni nini toba hiyo ambayo huleta mabadiliko makubwa ya akili na roho na matendo. Kazi ya mabadiliko lazima ianzie moyoni, na kudhihirisha nguvu zake kupitia kila uwezo wa kiumbe; lakini mwanadamu hana uwezo wa kuanzisha toba kama hii, na anaweza kupata peke yake kupitia kwa Kristo, ambaye alipaa juu, aliongoza mateka, na kuwapa wanadamu karama.” — *Selected Messages,* bk. 1, pp. 392, 393.

**b. Je, ni mamlaka gani ya uungu ambayo Kristo alifunua ambayo Alikuwa nayo? Yohana 5:25–29.**

“Kwa kuwa ameonja mpaka na masimbi ya shida na majaribu ya mwanadamu, na anaelewa madhaifu na dhambi za wanadamu; kwa sababu amestahimili kwa ushindi majaribu ya Shetani, na atashughulika na nafsi ambayo damu yake imemwagika ili kuiokoa, - kwa sababu hii, Mwana wa Adamu ameteuliwa ili kufanya hukumu.” — *The Desire of Ages*, p. 210.

“Kristo amewekewa uwezo wa kutoa uhai kwa viumbe vyote.” — *Selected Messages*, bk. 1, p. 249.

## 4. YESU, DHAMIRA KUU YA MAANDIKO 3/19 (Jtan)

**a. Je, Yesu alielezaje sababu ya kutokuamini kwa Wayahudi? Yohana 5:37, 38.**

---

"Badala ya kuomba radhi kwa kitendo walichokuwa wanamlalamikia, au kueleza sababu za kukifanya, Yesu aliwageukia wale wakuu, na mara mshtakiwa akageuka kuwa mshtaki. Aliwakemea kwa ugumu wa mioyo yao, na kutokujua kwao Maandiko. Alitamka kwamba walikuwa wamelikataa neno la Mungu, kwa kule kumkataa Yeye aliyetumwa na Mungu." — *The Desire of Ages,* p. 211.

**b. Kwa nini Wayahudi walishindwa kuelewa Maandiko? Yohana 5:39, 40.**

---

---

"Katika kila ukurasa, iwe ni historia, sheria, au unabii, Maandiko ya Agano la Kale yanaangazia utukufu wa Mwana wa Mungu. Kwa kuwa ulianzishwa na mbingu, mfumo wote wa Kiyahudi ulikuwa ni unabii wa injili. "Manabii wote humshuhudia" Kristo. Matendo 10:43. Tangu ile ahadi iliyotolewa kwa Adamu, na kushuka kupitia mtiririko wa wazee wa zamani na mfumo wao wa kisheria, nuru ya utukufu ya mbinguni iliweka alama za nyayo za Mkombozi. Watabiri waliiona Nyota ya Bethlehemu, Shilo ajaye, kadiri mambo ya usoni yalivyopita machoni pao katika mtiririko wa mafumbo. Katika kila kafara kifo cha Kristo kilionyeshwa. Katika kila wingu la moshi wa uvumba uliofukizwa haki yake ilipaa. Katika kila tarumbeta ya yubile iliyopigwa jina lake liliimbwa. Katika fumbo kuu la patakatifu pa patakatifu utukufu wake ulikaa.

"Wayahudi walikuwa na Maandiko mikononi mwao, na walidhani kwamba katika yale maarifa yao ya nje ya neno walikuwa na uzima wa milele. Lakini Yesu alisema, "Wala neno lake hamnalo likikaa ndani yenu." Wakishakumkataa Kristo katika neno lake, walimkataa yeye halisi katika umbo. Alisema, "Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima."

"Wakuu wa Wayahudi walikuwa wamejifunza mafundisho ya manabii kuhusu ufalme wa Masihi; lakini walikuwa wamefanya hili, si kwa hamu ya kweli ya kuujua ukweli, bali kwa lengo la kutafuta vigezo vya kuhalalisha tamaa zao kwa vitu vya kidunia. Wakati Kristo alipokuja katika namna inayotofautiana na matarajio yao, hawakuweza kumpokea; na kwa lengo la kuhalalisha msimamo wao, walijaribu kumwonyesha kama mwongo. Mara walipokuwa wameweka miguu yao katika njia hii, ilikuwa rahisi kwa Shetani kuimarisha upinzani wao dhidi ya Kristo. Maneno yale yale ambayo yangepokelewa kama uthibitisho wa uungu wake yalitafsiriwa dhidi yake. Kwa hiyo walibadili ukweli wa Mungu na kuufanya uongo." — *Ibid.*, pp. 211, 212.

## 5. UTUKUFU WA MUNGU — 3/20 (Alhamis)

**a. Ni nini kiliwafanya Wayahudi kumkataa Yesu na kutafuta walimu wa uongo? Yohana 5:41–44.**

---

“Yesu alisema, ”Mimi siupokei utukufu kwa wanadamu.” Hakutamani kuungwa mkono na Sanhedrin, wala kutumainia mamlaka hiyo. Hakupata heshima kutokana na idhini yao. Alikuwa amepewa heshima na mamlaka ya mbinguni. Ikiwa angetaka heshima, malaika wangekuja na kumpa heshima; Baba angekuwa pia amemthibitisha katika uungu wake. Lakini kwa ajili ya manufaa yao, kwa ajili ya taifa ambalo wao walikuwa viongozi wake, alitamani wakuu wa Wayahudi kuelewa tabia yake, na kupokea baraka ambazo alikuwa amekuja kuleta.

”Mimi nimekuja kwa jina la Baba yangu, wala ninyi hamnipokei; mwingine akija kwa jina lake mwenyewe, mtampokea huyo.” Yesu alikuja kwa mamlaka ya Mungu, akiwa katika sura yake, akilitimiza neno lake, na akiutafuta utukufu wake; lakini hakupokelewa na viongozi wa Israeli; lakini pindi ambapo wengine wangetokea, wakitaja kuwa na sifa za Kristo, lakini wakisukumwa na matakwa yao wenyewe na kutafuta utukufu wao wenyewe, wangepokelewa. Ni kwa nini? Ni kwa sababu yeye anayetafuta utukufu wake mwenyewe anatafuta kukidhi hamu yake ya kujitukuza juu ya wengine. Wayahudi wangeitikia mivuto kama hiyo. Wangempokea mwalimu wa uongo kwa kuwa angewasifu katika majivuno yao na kukubali mawazo na mapokeo waliyokuwa wakiendeleza. Lakini mafundisho ya Kristo hayakupatana na mawazo yao. Yalikuwa ya kiroho, na yalidai kuitoa nafsi kama kafara; kwa hiyo wasingeyapokea. Walikuwa hawamjui Mungu, na kwao sauti ya Mungu kupitia Kristo ilikuwa sauti ya mtu mgeni.

“Je, kitu kile kile hakiko kinarudiwa leo? Je, hawako wengi, hata viongozi wa dini, ambao wanaifanya mioyo yao kuwa migumu dhidi ya Roho Mtakatifu, wakifanya isiwezake kwao kuitambua sauti ya Mungu? Hawako wanalikataa neno la Mungu, ili wapate kushika mapokeo yao? ” — *The Desire of Ages,* pp. 212, 213.

## 6. MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI — 3/21 (Ijumaa)

1. Ni mamlaka na haki gani Kristo alidai?
2. Ni uhusiano gani umekuwepo kati ya Yesu na Baba?
3. Kristo ana nguvu gani za uzima?
4. Eleza Yohana 5:39.
5. Eleza tokeo la taifa la Kiyahudi kumkataa Yesu kuwa Masihi

Sabato, Marchi 29, 2025

**Somo la 13**

# Yesu kuwalisha Makutano

**FUNGU LA KUKARIRI:** "Lakini Yesu akawaambia, Hawana haja ya kwenda zao; wapeni ninyi chakula" (Mathayo 14:16).

**Inapendekezwa kusoma:** *Shuhuda ya kanisa,* vol. 6, pp. 341–348.

"Mara nyingi tunasita, tunakosa uhiari wa kutoa vyote tulivyo navyo, tukiogopa kutumia na kutumika kwa ajili ya watu wengine. Lakini Yesu ametuhimiza kwamba, "Wapeni ninyi chakula." Agizo lake ni ahadi; na nyuma ya hilo kuna uweza ule ule uliolisha umati wa watu kando ya bahari. " — *The Desire of Ages*, p.369.

## 1. NAFSI ZENYE NJAA — 3/23 (Jpil)

a. Kando na wanafunzi, ni nani wengine waliandamana na Yesu Alipovuka bahari ya Galilaya kabla ya Pasaka? Yohana 6:1,2.

"Kristo alikuwa amepumzika mahali pa faragha akiwa na wanafunzi wake, lakini wasaa huu adimu wa utulivu ulivunjika baada ya muda mfupi. Wanafunzi walifikiri kwamba walikuwa wamepumzika mahali ambapo wasingebughudhiwa; kumbe muda mfupi tu baada ya makutano kumkosa Mwalimu wa kimbingu, waliulizia, "Yuko wapi huyo?" Baadhi miongoni mwao walikuwa wameona uelekeo ambako Yesu na wanafunzi wake walikuwa wameelekea. Wengi walitembea kwa njia ya nchi kavu kuwaendea, wakati wengine walifuata kwa mashua kupitia majini. Pasaka ilikuwa imekaribia, na, kutoka mbali na karibu, makundi ya wasafiri waliokuwa njiani kwenda Yerusalemu walikusanyika kumwona Yesu. Idadi ya watu iliongezeka, mpaka wakakusanyika wanaume elfu tano bila kuhesabu wanawake na watoto. Kabla ya Yesu kufika pwani, makutano wengi walikuwa wanamsubiri. Lakini alifika ufukweni bila wao kumwona, na alitumia muda mfupi kwanza kuwa na wanafunzi wake pembeni. " — *The Desire of Ages*, p. 364.

b. Elezea hali ya kiroho ya watu wanaokusanyika. Marko 6:34.

## 2. KUJALI MAHITAJI YETU 3/24 (Jtatu)

**a. Yesu alitambua nini kwa upole ambacho watu walihitaji—na alitumiaje fursa hii kujaribu imani ya mfuasi Wake, Filipo? Yohana 6:3–6.**

“Kutokea kwenye mtelemko wa mlima[Yesu] alilitazama kundi lile kubwa la watu lililokuwa likisogea, na moyo wake ukajawa na huruma. Akiwa amebughudhiwa vile, na akiwa ameporwa nafasi ya pumziko lake, hakusubiri zaidi. Aliona hitaji kubwa la kutaka mwitikio wake kwa watu waliokuwa wanaendelea kuja. Naye “akawahurumia; kwa sababu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji.” Akiondoka katika mahali pake alipokuwa ametembelea, alitafuta mahali panapofaa ili aweze kuwahudumia. Hawakupata msaada kutoka kwa makuhani na wakuu; lakini maji ya uzima yanayoponya yalitiririka kutoka kwa Kristo kadiri alivyowafundisha makutano njia ya wokovu.....

“Siku ile ilikuwa kwao kama vile mbingu ilikuwa duniani, na hawakuwa na kumbukumbu kabisa kuhusu muda uliokuwa umepita tangu walipokuwa wamekula chakula.

“Muda mrefu wa siku ile ulikuwa umetumika. Jua lilikuwa linazama magharibi, lakini bado watu waliendelea kuwepo. Yesu alikuwa amefanya kazi siku nzima pasipo kula wala kupumzika. Alikuwa amedhoofu kwa uchovu na njaa, na wanafunzi walimsihi aache kushughulika na kazi. Lakini hakuweza kuwaacha makutano waliomsonga pande zote....

“Yeye aliyewafundisha watu njia ya kupata amani na furaha alizingatia mahitaji yao ya kimwili kama alivyozingatia mahitaji ya kiroho. Watu walikuwa wamechoka wakizimia. Kulikuwa na wazazi wenye watoto wachanga mikononi mwao, na watoto wadogo wakizing’ang’ania sketi za mama zao. Watu wengi walikuwa....

“Wengi walikuwa wamekuja kutoka mbali, na walikuwa hawajala kitu tangu asubuhi. Huenda wangeweza kununua chakula katika miji na vijiji vinavyozunguka mahali pale. Lakini Yesu akasema, ”Wapeni ninyi chakula,...... ”halafu akamgeukia Filipo, na kumwuliza, ”Tununue wapi mikate, ili hawa wapate kula?” Alisema hivyo ili kujaribu imani ya mwanafunzi. ” — *The Desire of Ages*, pp. 364, 365.

**b. Mwitikio wa Filipo ulikuwaje? Yohana 6:7.**

“Filipo akaitazama ile bahari ya vichwa vya watu waliokuwa wengi pale, na akafikiria jinsi isivyowezekana kuwapatia chakula cha kuwatosha wote. Akajibu kwamba mikate ya dinari mia mbili hata isingekaribia kutosha kuwagawia wote ili kila mmoja apate kidogo-kidogo. ”—Ibid.

## 3. CHOCHOTE KILICHOPATIKANA 3/25 (Jnne)

**a. Andrea alimpa Yesu habari gani—na Bwana aliwaelekeza wanafunzi wafanye nini? Yohana 6:8–10.**

---

---

"Yesu aliulizia kuhusu kiasi cha chakula ambacho kilikuwepo miongoni mwao pale pale. Andrea akasema, „Yupo hapa mtoto, yuna mikate mitano ya shayiri na samaki wawili, lakini hivi ni nini kwa watu wengi kama hawa?" Yesu aliagiza vitu hivyo viletwe kwake. Halafu aliwataka wanafunzi wawaketishe watu kwenye majani katika makundi ya watu hamsini au mia moja, ili kuwa na mpangilio, na ya kwamba wote wapate kushuhudia kile ambacho angefanya." — *The Desire of Ages*, p. 365.

**b. Elezea hatua ambazo Kristo alichukua katika kuzidisha chakula —na ni somo gani tunaweza kujifunza kutokana na hili. Mathayo 14:19; Marko 6:37–41; Yohana 6:11.**

---

---

"Yesu hakutafuta kuwavuta watu Kwake kwa kutosheleza tamaa ya anasa. Kwa makutano hayo makubwa, waliochoka na wenye njaa baada ya siku ile ndefu, ya kusisimua, chakula rahisi ilikuwa ni uhakikisho wa nguvu Zake na utunzaji Wake mwororo kwao katika mahitaji ya kawaida ya maisha. Mwokozi hajawaahidi wafuasi Wake anasa za ulimwengu; sehemu yao inaweza kufungwa na umaskini; lakini neno Lake limeahidiwa kwamba hitaji lao litatimizwa, na Ameahidi lililo bora kuliko jema la duniani—faraja ya kudumu ya uwepo Wake Mwenyewe." — *The Ministry of Healing*, pp. 47, 48.

"Katika muujiza huu, Kristo alipokea kutoka kwa Bwana; Aliwagawia wanafunzi, akawagawia watu, na watu mmoja kwa mwingine. Hivyo wote waliounganishwa na Kristo watapokea kutoka kwake mkate wa uzima, na kuwagawia wengine. Wanafunzi wake ndio njia iliyowekwa ya mawasiliano kati ya Kristo na watu " — *Ibid.*, p. 49.

**c. Ni irihe somo ry'umurimo nyakuri turi kwibutswa aha ngaha? Yesaya 61:6.**

---

---

"Wanafunzi wakamletea Yesu vyote walivyokuwa navyo; lakini hakuwaita kula. Aliwaambia wawagawie watu. Chakula kikaongezeka mikononi Mwake, na mikono ya wanafunzi, iliyomfikia Kristo, haikujazwa kamwe.hazina ndogo ilitosha kwa wote. Makutano yalipokwisha kulishwa, wanafunzi walikula pamoja na Yesu chakula cha thamani, kilichotolewa mbinguni." — Ibid.

## 4. UZURI WA KUSHIRIKIANA 3/26 (Jtan)

a. Tunapaswa kujifunza nini kutokana na maagizo muhimu ambayo Yesu alitoa baada ya kulisha umati? Yohana 6:12, 13.

---

---

---

“Wakati vikapu vya mabaki ya chakula vilipokusanywa, watu wale walifikiria habari ya wenzao waliokuwa nyumbani. Walitaka na wao wapate sehemu katika mkate uliobarikiwa na Kristo. Vile vilivyokuwa katika vikapu vile viligawiwa kwa umati ule wenye hamu, na vilipelekwa katika maeneo yote yalizunguka mahali pale. ” — *The Desire of Ages*, p. 368.

“Yesu aliwaambia wanafunzi wake, ‘Kusanyeni vipande vilivyosalia, kisipotee chochote.’ Yoh 6:12. Maneno haya yalimaanisha zaidi ya kuweka chakula kwenye vikapu. Somo lilikuwa la namna mbili. Hakuna kitu cha kupoteza. Hatupaswi kuruhusu kuteleza hakuna faida ya muda. Hatupaswi kupuuza chochote ambacho kingemnufaisha mwanadamu. Acha kila kitu kikusanywe kitakachosaidia mahitaji ya watu wenye njaa duniani. Kwa uangalifu huo huo tunaweka hazina ya mkate kutoka mbinguni ili kukidhi mahitaji ya roho. Kwa kila neno la Mungu tunapaswa kuishi. Hakuna alichosema Mungu ni cha kupotea. Hakuna hata neno moja linalohusu wokovu wetu wa milele ambalo tunapaswa kulipuuza. Hakuna neno hata moja litakaloanguka chini bure.” — *The Ministry of Healing*, p. 48.

**b. Hata inapoonekana kuwa jambo lisilofaa au haliwezekani, ni sifa gani ya Kikristo tunayoagizwa kusitawisha? Isaya 58:6–8; 1Petro 4:9.**

---

---

“Katika kila dharura tunapaswa kutafuta msaada kutoka Kwake ambaye ana rasilimali zisizo na kikomo kwa amri Yake....

“Tunapoona mahitaji ya maskini, wajinga, wanaoteseka, ni mara ngapi mioyo yetu inazama. Tunahoji, ‘Ni nini kinachofaa kwa nguvu zetu dhaifu na rasilimali ndogo ili kutimiza hitaji hili baya? Je, hatutangoja mtu fulani mwenye uwezo mkubwa zaidi aongoze kazi, au tengenezo fulani liifanye?’ Kristo asema, ‘Wapeni ninyi chakula.’ Tumia njia,wakati, uwezo ulio nao. Mletee Yesu mikate yako ya shayiri.

”Ingawa rasilimali zako hazitoshi kulisha maelfu, zinaweza kutosha kulisha mtu mmoja. Katika mkono wa Kristo wanaweza kuwalisha wengi. Kama wanafunzi, toeni kile mlicho nacho. Kristo atazidisha karama. Atalipa tegemeo la uaminifu, rahisi kwake. Kile ambacho kilionekana kuwa kidogo kitathibitika kuwa karamu tajiri.” — *Ibid*., ukurasa wa 49, 50.

## 5. MUUMBA NA MTOAJI WETU — 3/27 (Alham)

a. Ni sifa gani ya ajabu ya Mungu ambayo hatupaswi kusahau kamwe? Zaburi 37:25, 26; Wafilipi 4:19.

“Ni neema ya Mungu kwa sehemu ndogo ndiyo inayotosheleza yote. Mkono wa Mungu unaweza kuzidisha mara mia. Kutokana na rasilimali zake anaweza kutandaza meza nyikani. Kwa mguso wa mkono Wake Anaweza kuongeza riziki ndogo na kuwatosheleza wote. Uweza wake ndio ulioongeza mikate na nafaka mikononi mwa wana wa manabii...

“Yesu alipowaambia wanafunzi wake wapeni ninyi chakula, wakasema, Hatuna kitu zaidi ya mikate mitano na samaki wawili; tusipokwenda tukawanunulie watu hawa wote vyakula.’ Luka 9:13 . Hiyo ni nini kati ya wengi?

“Somo ni kwa ajili ya watoto wa Mungu katika kila zama. Wakati Bwana anapotoa kazi ya kufanywa, basi wanadamu wasisimame ili kuuliza juu ya usawaziko wa amri hiyo au matokeo yanayoweza kutokea ya juhudi zao za kutii. Ugavi mikononi mwao unaweza kuonekana kukosa haja ya kujazwa; lakini katika mikono ya Bwana itakuwa zaidi ya kutosha. . . .

“Hisia kamili zaidi ya uhusiano wa Mungu kwa wale ambao Amewanunua kwa kipawa cha Mwanawe, imani kubwa zaidi katika maendeleo ya kuendelea ya kazi Yake duniani—hili ndilo hitaji kuu la kanisa leo. Usiruhusu mtu yeyote asipoteze muda katika kudharau uchache wa rasilimali zao zinazoonekana. Mwonekano wa nje unaweza kuwa usio na matumaini, lakini nguvu na imani kwa Mungu itakuza rasilimali. Zawadi iliyoletwa Kwake kwa shukrani na kwa maombi kwa ajili ya baraka zake, atazidisha kama alivyozidisha chakula walichopewa wana wa manabii na makutano ya watu waliochoka.” — *Prophets and Kings*, pp. 241–243.

## 6. MASWALI YA KUTAFAKARI BINAFSI — 3/28 (Ijumaa)

1. Eleza mtazamo wa watu katika kusikiliza maneno ya Kristo.
2. Je,Bwana aliwapa mahitaji yao ya kimwili jinsi gani?
3. Je, tunajifunza nini kutokana na jinsi Kristo alivyoweka makutano katika mpangilio?
4. Je, nikumbuke nini kila niliposhawishiwa, “Wapeni ninyi kula”?
5. Taja nyakati ambazo utunzaji wa Mungu kwako ulikuwa wa ajabu sana.

# Sadaka za Sabato ya Kwanza




## Januari 4

kwa Kituo cha Madhumuni mengi cha Afya na Elimu nchini Paraguay

(Tazama uk. 4.)



## Februari 1

kwa Msaada wa Maafa Duniani

(Tazama uk. 25.)




## Machi 1

kwa Kituo cha Elimu cha "Watoto wa Tabia".

(Tazama uk. 46.)